# BARAZA KUU LA WAISILAM WA TANZANIA (BAKWATA)


**OFISI YA MUFTI WA TANZANIA**

**MAWASILIANO:0652405667/0764244867**

**www.bakwataonlineacademy.ac.tz**

**PROGRAMU YA MAFUNZO  KWA NJIA YA MASAFA**

# KOZI YA UONGOZI NDANI YA BAKWATA




***Mufti wa Tanzania Sheikh Mkuu Dokta Abubakari Zubeir***

***Enyi milio amini, mtii Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume  na wenye mamlaka juu yenu miongoni mwenu (***An-Nisa’: 59)

## YALIYOMO


UTANGULIZI ..... 4
MATARAJIO YA MODULI ..... 6
MADA KUU ZA MODULI ..... 6
UFAHAMU WA THAMANI YA TAASISI ..... 6
  MALENGO YA MADA ..... 6
KUUNDA JINA ZURI (REPUTATION, BRANDING, GOODWILL) ..... 7
FAIDA ZA KUUNDA JINA ZURI ..... 8
HADHI YA BAKWATA NA MADUMUNI YA KIKATIBA ..... 9
2.2 MADHUMUNI YA KIKATIBA YA KUNZISHWA BAKWATA ..... 12
UCHAMBUZI WA MADHUMUNI YA KIKATIBA ..... 13
SIFA ZA KIONGOZI KULINGANA NA KATIBA NA SIFA ZA JUMLA ..... 15
  SIFA ZA KIKATIBA ..... 15
  UCHAMBUZI WA SIFA ZA KIKATIBA ..... 15
DIRA, DHAMIRA NA TUNU ..... 20
  DIRA YA BAKWATA (VISION) ..... 20
  DHAMIRA  YA BAKWATA(MISSION) ..... 21
  TUNU ZETU BARAZA (OUR CORE VALUES) ..... 21
  Uchambuzi wa kina juu ya tunu za BAKWATA. ..... 22
BAKWATA NA MIPANGO ..... 24
    UTANGULIZI ..... 24
    NADHARIA YA KAZI ZA UONGOZI(MENEJIMENTI) ..... 24
    MIPANGO NA USHAHIDI KUTOKA KATIBA YA BAKWATA ..... 25
UPANGAJI WA MIPANGO ..... 26
    NAMNA YA KUPANGA ..... 26
UTHUBUTU WA KUWEZA KATIKA MIPANGO ..... 27
    UTANGULIZI ..... 27
    MIFANO YA MIPANGO ..... 27
    KUTHUBUTU KUPANGA ..... 29
CHANGAMOTO ZA MIPANGO NDANI YA BAKWATA ..... 29
UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MIPANGO ..... 30
NIDHAMU NDANI YA BAKWATA ..... 32
    UTANGULIZI ..... 32
    NIDHAMU KWA MJIBU WA QUR AN  NA SUNNAH ..... 33
    NIDHAMU YA KWA MUJIBU WA KATIBA YA BAKWATA ..... 33
    NIDHAMU KWA VIONGOZI ..... 33
    NIDHAMU YA NGAZI ZA JUU ..... 33
    MADHARA YA KUKOSEKANA KWA NIDHAMU ..... 35

NJIA ZA KUREJESHA NIDHAMU ........................................................................................35
MAANDALIZI YA VIONGOZI KUPITIA DAARUL MAARIF .......................................................36
AZIMIO LA KUANZISHA DARUL MA'ARIF..................................................................................36
UCHAMBUZI WA KAULI MBIU YA JITAMBUE, BADILIKA, ACHA MAZOEA .......................37
UTANGULIZI ........................................................................................................................37
MAANA YA KAULI MBIU NA UMUHIMU WAKE ...........................................................37
UMUHIMU WA KAULI MBIU ...............................................................................................38
UCHAMBUZI WA KAULI MBIU YA JITAMBUE, BADILIKA , ACHA MAZOEA .............38
JITAMBUE.................................................................................................................................38
BADILIKA ...............................................................................................................................39
ACHA MAZOEA .......................................................................................................................40
MFUMO NA KAULI MBIU YA JITAMBUE, BADILIKA, ACHA MAZOEA ........................40
MALI ZA BAKWATA, UPOKEAJI WA WAQFU NA MATUMIZI YA WAQFU ...........................42
UTANGULIZI ........................................................................................................................42
UFAHAMU KUHUSU BARAZA LA WADHAMINI ........................................................................42
MAANA YA BODI YA WADHAMINI....................................................................................42
KAZI ZA BODI YA WADHAMINI KWA UJUMLA ...............................................................42
UFAHAMU KUTOKA KATIKA KATIBA YA BAKWATA.....................................................43
Ibara ya 69. BARAZA LA WADHAMINI. ..............................................................................43
MALI YA BAKWATA ..................................................................................................................44
WAQFU .......................................................................................................................................44
MAANA YA WAQFU ..............................................................................................................44
WAQFU KATIKA BAKWATA ................................................................................................44
UPOKEAJI WA MALI ZA WAQFU ZA BAKWATA..............................................................44
MFANO WA MAANDISHI YA KUTOA WAQFU ..................................................................46
UCHAMBUZI WA HALI YA BAKWATA (SWOT ANALYSIS). ...................................................50
MAZINGIRA YA NDANI YA BAKWATA (NGUVU NA UDHAIFU)....................................51
NGUVU ZA BARAZA (STRENGTHS)..........................................................................................51
MAZINGIRA YA NJE YA BAKWATA(FURSA NA TISHIO) ................................................52
TISHIO/VIKWAZO KWA BARAZA (Threats/challenges)........................................................53
MAJUKUMU YA KUFANYA UCHAMBUZI WA HALI BAKWATA (SWOT ANALYSIS). 53
UCHUMI NDANI YA BAKWATA NA USIMAMIZI WA FEDHA...............................................53
a) KUHIMIZA NA KUSAIDIA ...................................................................................................53
b) MIRADI, UCHUMI, UZALISHAJI MALI ...............................................................................54
UCHUMI .......................................................................................................................................54
MAANA YA MRADI ................................................................................................................54
MRADI WA KIUCHUMI .........................................................................................................55
USIMAMIZI WA FEDHA.........................................................................................................55

MASWALA YA USIMAMIZI WA FEDHA KWA MUJIBU WA KATIBA YA BAKWATA .......... 55
MASWALA YA FEDHA KATIKA NGAZI ZA KIUTAWALA ZA BARAZA ........................ 56
MAMBO YANAYOHUSU UHASIBU ........................................................................ 57
MWAKA WA FEDHA WA BARAZA ........................................................................ 57
MISINGI YA UHASIBU ........................................................................................ 57

**UTANGULIZI**

Moduli hii ni maalumu kwa viongozi ambao wapo katika nafasi mbali mbali za BAKWATA kwa sasa na wale ambao si viongozi lakini wangependa kusoma kwa matumizi yao ya baadaye.

Uandaaji wa moduli hii unatokana na ukweli kwamba moduli za kwanza za kozi ya UONGOZI, UTAWALA BORA NA TEHEMA ziko katika hali ya ujumla sana. Hivyo kuwezo kuleta ufanisi wa kina kwa mtendaji moduli hii itaongeza chachu kubwa katika kutambua zaidi baraza na kujenga uhalisi kuliko upotoshaji ambao umevizwa kwa muda mrefu na watu. Kila mpotoshaji amejitahidi kupotosha kuwa BAKWATA haiwezi kufanya jambo lolote la maana isipokuwa litakwama. Hii ni dhana ya watu waovu ambao wapo ndani ya nafasi za BAKWATA kuwakatisha watu tamaa na wao wenyewe hawataki kuwa na MABADILIKO.
Mfano halisi wa moduli hii ni kama watu waliosoma masomo ya uhandisi (Engineering), lakini wakajengewa ujuzi maalumu katika uhandisi maalumu (Specilization). Kama vile uhandisi wa majengo, uhandisi wa umeme, uhandisi wa elektonic n.k. Maanake ni kuwa kusomea kwa kina masomo maalumu juu ya uongozi ndani ya BAKWATA ni kumjenga zaidi kiongozi kuwa na weledi mpana wa kazi katika maswala ya ndani ya BAKWATA.

Mheshimiwa MUFTI ABUBAKARI ZUBERI katika kuleta kwake kauli mbiu (SLOGAN) ya JITAMBUE, BADILIKA ,ACHA MAZOEA alilenga kupambana na upotoshaji ambao ulilemaza akili za watendaji kwa muda mrefu. Umezaji wa akili huu umefanya badala ya kutatua changamoto za ndani ya BAKWATA , viongozi hao hao wanageuka kusema vibaya maswala ya BAKWATA pasina kutafuta majibu muafaka. KUSEMA bila kutenda ni MAKOSA. Taasisi zote duniani zinazo changamoto zinazozikabili, na kwa kitaalam huwa inaitwa uchambuzi wa hali halisi ya taasisi (yaani SWOT analysis). Uchambuzi wa kina wa SWOT utafafanuliwa katika moduli hii. SWOT ni kifupi cha S(Strength), W(Weekness),O(Opportunity) and T(Threats).





**MATARAJIO YA MODULI**

Matarajio ya moduli hii mwisho msomaji anatarajiwa kuwa;

1. Kujengeka katika fikra safi za utendaji na siyo kulalamika bila kutafuta majawabu ya changamoto husika.
2. Kujenga ufahamu wa pamoja kuhusu BAKWATA katika kukabaliana na upotoshaji wa makusudi wa watu ndani ya BAKWATA yenyewe.
3. Kutekeleza madhumuni ya kikatiba ya BAKWATA.
4. Kuleta mshikamano ndani ya BAKWATA unaotokana na elimu sahihi.

**MADA KUU ZA MODULI**




Mada kuu za moduli hii ni;

1. UFAHAMU WA THAMANI YA TAASISI
2. HADHI YA BAKWATA NA MADHUMUNI YA KIKATIBA
3. SIFA ZA KIONGOZI WA BAKWATA KIKATIBA
4. DIRA , DHAMIRA NA TUNU ZA BAKWATA
5. BAKWATA NA MIPANGO
6. UTHUBUTU WA KUWEZA KATIKA MIPANGO
7. NIDHAMU NDANI YA BAKWATA
8. MAANDALIZI YA VIONGOZI KUPITIA DARUL MAARIFA
9. UCHAMBUZI WA KAULI MBIU YA JITAMBUE, BADILIKA, ACHA MAZOEA
10. MALI ZA BAKWATA, UPOKEAJI WA WAQFU NA MATUMIZI YA WAQFU
11. UCHAMBUZI WA HALI YA BAKWATA (SWOT ANALYSIS).
12. UCHUMI NDANI YA BAKWATA NA USIMAMIZI WA FEDHA

**UFAHAMU WA THAMANI YA TAASISI**




**MALENGO YA MADA**

Jina kubwa la BAKWATA, mtandao mkubwa wa BAKWATA nchini Tanzania(Kutoka Taifa hadi Msikiti) , uwezo mkubwa wa BAKWATA unatakiwa kuchukuliwa kama FURSA ya kujiletea maendeleo nchini. Kinyume chake ni kuona uhalisia haupo kama jina kubwa lilivyo, mtandao ulivyo na uwezo wake. Hii ni kutokana na vipimo vya kitaalam vya kupima THAMANI ya taasisi yoyote duniani. THAMANI (Value) ya taasisi inapimwa kwa kuthaminisha rasilimali zinazoshikika (Tangible assets) na zisizoshikika (Intangible assets).

Lengo kuu la moduli hii kwa msomaji wa uongozi ni kujenga ufahamu wa kina juu ya kuipa THAMANI halisi BAKWATA kwa kuanzia kutoka ilipo kwenda mbele kwa miaka mingine mitano, au kumi au ishirini. Vigezo vya kupima thamani ya taasisi si maneno na porojo za hapa na pale. Taasisi yoyote duniani inapimwa thamani yake kwa kuwa na JINA ZURI(Reputation) na kuwa na MALI (assets) za kutosha. Jinsi ya kutambua jina zuri na kupima assets za taasisi ndiyo maana ya kuandaliwa kwa moduli hii.

**MAANA YA MANENO MUHIMU**

1.1.1 **Mali (assets) :** Ni jumla ya vitu vyote vinavyomilikiwa na taasisi.

1.1.2 **Mali zinazoshikika (tangible assets):** Ni zile mali ambazo zinashikika. Mfano wake ni magari, nyumba, viwanja, n.k.

1.1.3 **Mali zisizoshikika (intergible assets) :** Hizi ni mali ambazo huwezi kuzishika wala huwezi kuzigusa ukazishika. Hizi ni mali ambazo zina thamani kubwa sana katika taasisi. Mfano ni JINA ZURI (Reputation, Brand, Goodwill), Haki miliki (Copy right).

Angalizo***: Ni somo pana sana kuweza kuchambua kuhusu mali hizi zisizoshikika. Lakini hapa katika kutambua umuhimu mkubwa wa jina zuri lazima msomaji wa moduli hii ufahamu kuwa kutengeneza jina zuri ni swala la maamuzi ya watu wa taasisi wenyewe kujiweka katika sifa nzuri za kuipaisha taasisi yenyewe. Kwa mfano , hakuna mahala popote katika katiba ya BAKWATA kuna ibara ambayo inachochea watu kuita au kujenga jina baya kwa BAKWATA, ni utashi wa mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu ndani ya BAKWATA ambao wamekata tamaa au hawana ujuzi wowote wanaoamua kuchafua BAKWATA. Mambo muhimu katika moduli hii yatasaidia kubadili fikra za watu wanaochafua bila kujua au kwa kujua kuwa hakuna mahala popote taasisi duniani inaamka na kuwa na jina zuri kama halijatengenezwa na wenye taasisi. Hii Jitambue , badilika, acha mazoea ni moja ya kauli mbiu za kurejesha JINA ZURI kwa kufanya mambo mazuri. Mambo mazuri kikatiba yapo.***


## KUUNDA JINA ZURI (REPUTATION, BRANDING, GOODWILL)




Kama ilivyofafanuliwa hapo juu kuwa jina zuri la taasisi ni mtaji wenye thamani kubwa kwa taasisi. Njia kubwa inayotumika kuunda jina zuri kwa taasisi nyingi duniani ni UAMINIFU(trustful). Hii ni kwa taasisi zote. Kwa watumishi ndani ya BAKWATA kuna neno la jumla ambalo wanatakiwa kujipamba nalo ili kuunda jina zuri ambalo ni UCHAMUNGU. Uchamungu ni zaidi ya uaminifu.

Mchamungu anakatazika na yale yote ambayo Mungu ameyakataza na anayakimbilia yale yote ambayo Mungu ameyaamrisha. Hapa maana katika taasisi ambazo zinafanya biashara, inaweza kuwa biashara hiyo ni haramu kwa mujibu wa makatazo ya Mwenyezi Mungu, lakini wao wanaendesha mambo kwa kuaminiwa sana na wanaowahudumia, na hivyo wakajenga jina zuri kwa wateja wao. Kwa hali hii mtumishi ndani ya BAKWATA hata kama atafanya juhudi kubwa namna gani, kujenga jina zuri la BAKWATA , lazima namba moja katika nafsi yake atangulize UCHAMUNGU kwanza. Anaweza kufanya mambo makubwa lakini kwa nia ya kutaka asifiwe na binadamu na kujionyesha (ria). Hii ni katika madhambi, hivyo ulazima wa kuwa wachamungu katika utendaji, hakika lazima jina zuri la BAKWATA litapatikana na kudumu kila kona ya nchi.

**TAFAKURI YA MADA**




1. ***Je, wewe ni kiongozi unayejipamba na sifa za uchamungu?***
2. ***Je , wewe ni kiongozi unahakikisha BAKWATA inapata jina zuri kutokana na utendaji wako?***
3. ***Je, wewe ni kiongozi unayehakikisha jina zuri la BAKWATA linajengwa katika mahala pako unapoishi?***

## FAIDA ZA KUUNDA JINA ZURI

### i. Kupata radhi za Allah

Hii maana yake kuwa kiongozi ndani ya BAKWATA kama atafanya kazi kwa kuzingatia uchamungu wake, kwanza atapata radhi za Allah na pili ataipa BAKWATA jina zuri. Kwa maana hii kiongozi mwenye nia ya kuipa BAKWATA jina zuri ambaye pia amejipamba na uchamungu, faida kubwa zaidi ya yote atapata radhi za Allah. Je, kuna kiongozi anahangaika kufanya kazi ndani ya BAKWATA ili achume moto na siyo kupata radhi za Allah? Kama yupo kiongozi wa namna hii wa kutafuta moto, basi moduli hii kwa idhini ya Allah iweze kumzindua na kuacha mara moja yale yasiyomridhia Allah na kuipa jina zuri BAKWATA.

### ii. Kupata kuaminiwa na watu

Jina zuri ni mtaji mkubwa zaidi ya fedha. Hujawahi kuona au kusikia kauli za mtaani kuwa ; Sheikh nifanyie Uisilam?. Watu wanatumia kama neno Uisilam ni dini safi ya waaminifu. Hii

katika faida kubwa sana ya kuaminiwa na watu, maana yake kuwa jamii ya ndani na ya nje inapendezwa na huduma zinazotolewa. Ni jukumu la kiongozi mmoja mmoja au katika kikundi kuhakikisha wanajenga jina zuri kwa faida ya kupata kuaminiwa na watu.

Viongozi waliojitahidi kufanya kazi kwa uadilifu, walipata kuaminiwa na watu na hatimaye wakafanya maendeleo makubwa sana ya kupigiwa mfano. Kuna mahala pengi viongozi wa BAKWATA wamelipa heshima baraza kwa uaminifu wao wa kusimamia mali za umma na wakaona matunda yake. Ipo pia mifano michafu ya viongozi wasiokuwa waadilifu wamefanya mambo ya hovyo na kuharibu jina la baraza mahala hapo. Kwa hali hii kila mahala nchini viongozi wa BAKWATA wajikague mifumo yao ya kufanya kazi wataaminiwa na watu watafanya maendeleo makubwa kama sehemu ambazo ipo mifano ya wazi.

### iii. Kufanya maendeleo makubwa kwa muda mfupi

Hii inatokana na uchamungu, kisha watu wakaamini uongozi na kwa uhakika kidogo kidogo kinachotokana na watu wengi kinaleta maendeleo makubwa kwa muda mfupi sana. Hii sasa kila mahala wahusika waweze kujisafisha nafsi zao na kuweka AZMA kuwa wanataka maendeleo makubwa kwa muda mfupi kwa kuwa tayari wamewekeza mtaji wa jina zuri.

### iv. Kupata maendeleo ya kudumu

Maendeleo ya kudumu ni yale ambayo yatakuwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine yanazidi kuwa makubwa na siyo ya kuporomoka kurudi nyuma. Maendeleo haya kama yamepatikana kwa misingi imara kutoka mwanzo hayatii ugumu wa kudumu kwake. Jina zuri la taasisi linatokana na mifumo madhubuti ya utendaji wake. Kama kuna mifumo madhubuti haitakuwa na ugumu wa kurithisha mambo mazuri yanayotokana na jina zuri la taasisi, hivyo kwa hali hii matarajio ya maendeleo ya kudumu yanakuwa makubwa sana.

### v. Kuipatia jamii maisha bora na yenye amani

Madhumuni ya kuundwa kwa taasisi kama BAKWATA katika katiba yenyewe yamejipambanua moja kwa moja. Madhumuni yote yamekusudia kuipatia jamii maisha bora na yenye amani. Hii maanake ni kuwa kutimiza azma ya jina zuri kwa utendaji uliotukuka, lazima jamii itanufaika na matunda ya kuwepo kwa taasisi. Je, katika misikiti, mitaa/kata, katika wilaya na mikoa hali ya jamii kunufaika ikoje katika sekta ya elimu, afya, uchumi na sekta zingine mbali mbali?

**HADHI YA BAKWATA NA MADUMUNI YA KIKATIBA**

## 2.0 MALENGO YA MADA

Utafiti rasmi wa kitalaam ambao umewahi kufanyika katika Mkoa wa KAGERA mwaka 2018 ulibaini kuwa kwa viongozi 10 wa BAKWATA , kati yao 7 hawana katiba na hawajui majukumu yao ya kikatiba. Maanake ni viongozi watatu kila kundi la viogozi 10 ndiyo wenye katiba na wanajua majukumu yao ya kikatiba. Huu ulikuwa ni utafiti rasmi ambao ulifanyika kwa viongozi kujaza dodoso maalumu kasha watalaam wakachambua. Utafiti huu kama mfano (Sample) unaweza kubeba taswira ya viongozi katika mikoa 26 ya Tanzania. Hali

ikoje kwa MKOA wako? Hali ikoje kwa Wilaya yako ? Hali ikoje kwa kata yako? Hali ikoje katika msikiti wako?




Kuchambua mada hii kwa ufupi sana kutamjengea kiongozi wa BAKWATA ufahamu wa awali wa kufahamu maeneo walau muhimu ya Katiba na kumjengea uwezo mkubwa wa kutafuta katiba ya BAKWATA ya mwaka 1999 toleo la mwaka 2018.


### 2.1 HADHI

Kutoka katika katiba ya BAKWATA sehemu ya kwanza tunakuu kifungu cha tano (5) kama ifuatavyo;

Kifungu cha 5; ***"Msingi wa maongozi yote ya Baraza Kuu na utekelezaji wake na shughuli zake zote mbalimbali utakuwa wa kitabu cha Mwenyezi Mungu(Qur-aani)na Sunna za Mtume Muhammad s.a.w."***

Kwa nukuu hapo juu, maanake kiongozi wa BAKWATA katka ngazi yoyote ile anatakiwa kufahamu kuwa kabla ya katiba ya BAKWATA anafahamu QUR AN NA SUNNA ZA MTUME MUHAMMAD (s.a.w)?
Kwa muda mrefu viongozi walio wengi ndani ya BAKWATA wamejenga taswira kama BAKWATA ni chombo cha kufanya FITINA mbaya wao kwa wao pasina kuzingatia UTU na HESHIMA kubwa ya UISILAM iliyofafanuliwa katika QUR AN na SUNNA za Mtume (s.a.w). Kuweza kupambika na sifa za kuwa kiongozi bora wa BAKWATA kwa nukuu ya kifungu cha 5 , kiongozi hana budi kuzingatia hatua kubwa mbili;

i. Kuijua QUR AN na kuzijua Sunna za mtume(S.A.W)
ii. Baada ya kuijua lazima sasa aweze kuitekeleza kwa kuiishi kwa matendo na kuzitekeleza sunna.




Kumekuwepo na viongozi wajuzi wa mambo na wasomi wazuri wa dini lakini wameharibika na makundi maovu yanayowapotosha kuishi kwa fitina na husuda nyingi. Kwa masomo ya moduli hii ni wajibu sasa kila kiongozi kujitakafakari mwenye kwa nukta zifuatazo;


i. Lengo lake kuumbwa analifahamu?
ii. Kama lengo la kuumbwa analifahamu anajua ipo siku atakufa?
iii. Je, kama anatambua kuwa atakufa anajua kuwa kuna siku ya mizani yake kuhesabiwa na kulipwa malipo?
iv. Je, anatambua kuwa kuna MOTO na PEPO?

Ufahamu mbaya kuhusu BAKWATA unaanzia katika msingi wa kutofahamu sawa sawa QUR AN na Sunna na pia kushindwa kwa kiongozi kufuata QUR AN na Sunna na hata baada ya kujua. Moduli hii inakumbusha na kumrejesha kiongozi katika msimamo wa sawa sawa. Ni jukumu la kiongozi kurejea kuwa hakuna miujiza katika hili la kujiweka karibu sana na Allah kwa kuwa tayari Allah katoa maelekezo yake katika QUR AN aya ya 11 ya Surat Ra'ad (13) isemayo:

***"……..Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo naf-sini mwao………"***

Kiongozi mmoja mmoja kama anataka kupata PEPO kwa kupitia kazi za BAKWATA hana budi kujua ni jukumu lake binafsi kusafisa nafsi yake kwa kubadili yale makando kando yote machafu ya kuwapiga watu FITINA na kuwakandamiza kwa kujisifia ndiyo bingwa wa vitimbi viovu ndani ya BAKWATA. Kujipamba na sifa chafu si HADHI ya BAKWATA halisi kwa kuwa tayari BAKWATA halisi kikatiba imejipmbanua makuzi na malezi ya maongozi yanafuata QUR AN na sunna.

**TAFAKURI YA MADA**





1. ***Je, wewe ni kiongozi unayefahamu QUR AN na SUNNA?***
2. ***Je , wewe ni kiongozi unayefuata QUR NA na SUNNA?***
3. ***Je, wewe ni kiongozi unayejikweza kuongoza Waisilam kwa kuvunja maongozi ya QUR AN na SUNNA na unataraji PEPO?***

Kiongozi afanye nini ili aweze kuwa kiongozi bora wa BAKWATA halisi ya kumpeleka peponi na siyo BAKWATA ya kujiundia MOTO?

i. Ajifunze QUR AN na SUNNA kwa bidii
ii. Aweze kuishi maisha ya QUR NA NA SUNNA akitaraji kupata pepo ya ALLAH
iii. Ajinasue na marafiki wabaya Katika BAKWATA ambao kwa muda mrefu wamempotosha
iv. Afanye toba kwa makosa yake yaliyopita na kujipamba na mambo mema
v. Atoe sana sadaka
vi. Aswali swala la usiku kuujenga moyo wake
vii. Afanye adhikari sana kwa yakini, si adhikari bila mazingatio.

Kwa machache yaliyotajwa hapo juu na mengine mengi ambayo anaweza kuyapata kwa wanazuoni mbali mbali, kingozi wa BAKWATA lazima atakuwa bora sana kuyatekeleza majukumu yake ya kikatiba.

## VIELELEZO VYA KUHITIMISHA




**2.2 MADHUMUNI YA KIKATIBA YA KUNZISHWA BAKWATA**

Katiba ya Bakwata imeweka madhumuni yanayoakisi masilahi ya Uislamu na Waislamu nchini kama yanavyobainishwa katika Ibara ya 9 (1-17) kuwa:

1. Kusimamia, kufungua, kujenga, na au kusaidia na kuendesha vyuo vya dini na elimu ya dunia kwa Waislamu wa Tanzania, na kutoa uwezo wa elimu ya juu kwa wanafunzi wa Kiislamu.
2. Kusimamia na kutetea haki za msingi za Waislamu nchini, na kukemea mambo yanayoleta kero kwa Waislamu.
3. Kuanzisha na kuhimiza Tabliigh ya dini na kueneza dini katika lugha ambazo BARAZA limezitaja katika Katiba hii.
4. Kusimamia malezi na maadili mema kwa vijana wa Kiislamu na Waislamu kwa ujumla.
5. Kuwahimiza na kuwasaidia Waislamu nchini kuanzisha miradi na shughuli za uchumi na uzalishaji mali kwa lengo la kuupiga vita umaskini.
6. Kufungua, kujenga, kusimamia, na au kusaidia kuendesha misikiti, mali za wakfu, huduma za afya na matibabu kama BARAZA litakavyoona inafaa.
7. Kusimamia, kuhimiza, kuimarisha, na au kusaidia kuweka mipango ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa Zakka na Sadaka kwa kutimiza amri ya Mwenyezi Mungu, na katika kuinua dini na maendeleo ya Waislamu.
8. Kusimamia, kuendesha, na au kusaidia kuendesha mipango ya utunzaji na malezi kwa watoto yatima, watu wasiojiweza na maskini.
9. Kusimamia, kuhimiza, na au kuweka taratibu na mipango ya 'Hijja na Umra' na huduma zake.
10. Kusimamia, kuendesha, na au kusaidia kuweka mipango ya Ndoa, Talaka, Mirathi na haki ya kurithi mali za Waislamu zilizoachwa bila ya wenyewe.
11. Kuweka mipango ya kusimamia utekelezaji wa Ibada za Kiislamu na sherehe za sikukuu za kidini, kama siku ya kuzaliwa Mtume Muhammad (S.A.W), sikukuu za Idd, sikukuu ya Mwaka Mpya na inapendekezwa kuwa siku hiyo ya mwaka mpya wa Kiislamu iwe siku ya mapumziko kitaifa.
12. Kutoa au kupokea misaada kwa ajili ya maendeleo, kudumisha mila na utamaduni wa Kiislamu, na ustawishaji wa hali njema za Waislamu wa Tanzania.

13. Kuweka uhusiano na ushirikiano kati ya Bakwata na Waislamu wa nchi nyingine, na kuishi kwa amani na watu wa dini mbalimbali nchini Tanzania.
14. Kukopa toka Benki au taasisi za fedha za ndani au nje ya nchi, kukopesha, kununua, kuuza, kuhamisha, kuondosha, kuweka rehani, kujenga, na au kuwa na haki juu ya ardhi kwa ajili ya kutimiza shabaha na madhumuni ya Baraza Kuu la Waislamu wa Tanzania (Bakwata).
15. Kuanzisha Miradi ya Uchumi na uzalishaji mali na kuwekeza katika taasisi za rasilimali.
16. Kupokea Sadaka na Misaada ya vitu mbalimbali kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi, kwa madhumuni ya kuendeleza shughuli za Bakwata.
17. Kukagua na kupokea taarifa kutoka katika taasisi zote za Kiislamu nchini.

## UCHAMBUZI WA MADHUMUNI YA KIKATIBA


Kuwepo kwa madhumuni ya katiba yoyote ile katika taasisi kuna kazi kubwa mbili;

i. Kupata ridhaa ya kusajiliwa serikalini
ii. Kutekeleza madhumuni ya kikatiba katika kuleta maendeleo

Tayari BAKWATA imesajiliwa serikalini kwa serikali kuridhia madhumuni hayo yatekelezwe katika kuwaletea jamii maendeleo.
Mafumo bora wa kikatiba ya BAKWATA umetambua kuwepo kwa ngazi kuu tano ambazo ni ngazi ya TAIFA, ngazi ya MKOA, ngazi ya WILAYA, ngazi ya KATA na ngazi ya MSIKITI.
Katika kila ngazi kuna mamlaka ya kikatiba ya kuchambua na kuona namna ya kutekeleza madhumuni ya kikatiba kulingana na upatikanaji wa rasilimali na uchambuzi wa kina wa kuwashirikisha wadau katika kufanikisha madhumuni. Hii maanake ni kuwa utekelezaji wa madhumuni ya kikatiba ndiyo shughuli za msingi za BAKWATA ZA kila ngazi. Kushindwa kutekelezwa kwa madhumuni hayo kuna mambo yanayoweza kuwa yanachangia kama vile;

i. Kutofahamika kwa madhumuni hayo ya kikatiba
ii. Kutofanyiwa uchambuzi wa kina na ngazi husika ya kikatiba
iii. Kukatishwa tamaa kwa muda mrefu kwa kuona hakuna jambo linalowezekana kufanyika katika BAKWATA.

**TAFAKURI YA MADA**




1. ***Je, wewe ni kiongozi ulikuwa unafahamu madhumuni ya kikatiba ya BAKWATA?***

2. ***Je, umefanya uchambuzi wa madhumuni yapi ya kikatiba ya BAKWATA ambayo unaona yanawezekana kutekelezeka katika mazingira yako?***

***3. Je, unadhani kuwa unaweza kukaa na wenzako katika ngazi yako ya uongozi mkafanya uchambuzi wa madhumuni yanayowekezekana?***

**MFANO WA CHATI YA KUFANYA UCHAMBUZI WA MADHUMUNI**

a) MADHUMUNI YANAYOTEKELEZWA KWA SASA

| **Dhumuni namba** | **utekelezaji wa sasa** | **Uwezo unaowezekana** | **Mikakati ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji** |
|---|---|---|---|
| Namba 1 | Tumejenga madrasa 10 katika kata yetu | Tunao uwezo wa kujenga madrasa za kisasa 25 | 1.Kuhamasisha waisilamu kujitolewa<br>2. Kuunda task force ya maendeleo ya ujenzi wa madrasa |
| Namba 15 | Miradi ya kiuchumi 5 imeanzishwa katika wilaya | Miradi 15 inaweza kuanzishwa | 1. Kununua mashamba<br>2. Kujenga vyumba vya maduka<br>3. Kuanzisha mashamba ya miti |

b) MADHUMUNI YANAYOWEZA KUTEKELEZWA BADO HAYAJATEKELEZWA

| **Dhumuni namba** | **Uwezo unawekana** | **Mikakati ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji** |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |

c) MADHUMINI YASIYOWEZEKANA KUTEKELEZWA

| **Dhumuni namba** | **Sababu za kutokutekeleza** |
|---|---|
| | |
| | |
| | |

**SIFA ZA KIONGOZI KULINGANA NA KATIBA NA SIFA ZA JUMLA**

MALENGO YA MADA

Kuzifahamu sifa hizi kunamlazimu kwanza kiongozi husika kujichunguza na kujipamba nazo. Lakini pia mamlaka zinazohusika na upekuzi (vetting) wa kuteua viongozi wanatakiwa kuzidi kuzingatia sifa hizi kwa kina na siyo kuweka mapenzi binafsi katika kupata viongozi bora watakaofanya shughuli zitakazopelekea kutimia kwa madhumuni ya kuundwa kwa BAKWATA.

**SIFA ZA KIKATIBA**

Kutoka katika sehemu ya nne, Ibara ya 79. SIFA ZA VIONGOZI WA BARAZA KUU LA WAISLAM WA TANZANIA (BAKWATA).

Viongozi waBaraza Kuu la **Waislam** wa Tanzania **(BAKWATA)** kuanzia ngazi ya Msikiti hadi ngazi ya Taifa, kama wanavyoelezwa katika Katiba hii ni lazima wawe:-

1. Waislam
2. Wanaume na Wanawake kwa wanawake wenzao.
3. Baalegh.
4. Wasiwe wendawazimu.
5. Wasiwe Mafaasiq.
6. Wawe wacha-Mungu na Waadilifu.
7. Wawe wenye kuchunga murua.
8. Wawe wenye himma katika Dini.
9. Wawe ni ahlu Sunna Waljama'a.
10. Wawe ni wenye kuikubali, Katiba ya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania na miongozo yake.

**Ibara ya 80.** Kiongozi yeyote atakayepoteza mojawapo kati ya sifa hizo kumi **(10)** atakuwa amepoteza uongozi wake.

**UCHAMBUZI WA SIFA ZA KIKATIBA**


Kwa kuwa vigezo vya kumpata kiongozi ndani ya BAKWATA viko wazi kikatiba, kukosekana kwa viongozi wenye sifa maanake ama wanaohusika na zoezi la kupata viongozi hawajawa makini na vigezo vya kikatiba au wanachaguliwa na kuteuliwa wao wenyewe hawajipimi katika kuifahamu katiba. Kama mwanzo wa moduli hii ilivyotangulia kufafanua kuwepo kwa OMBWE kubwa la viongozi wengi kutokuwa na katiba na wengine kutojua kabisa majukumu ya kikatiba. Uchambuzi huu unakusudia kuibua maarifa kwa wahusika ambao kwa sasa ni viongozi na wale ambao wanahusika na uteuzi wa viongozi.

Pamoja na kuzingatia sifa hizi ambazo zinachambuliwa hapa chini, ni jukumu la kiongozi husika kujua kuwa utambuzi wa mambo yeye binafsi na kujua majukumu ya uongozi ataulizwa kwa Allah ni vyema akawa ni mwenye kujipima zaidi na kujikagua nafsi yake.

**Sifa ya 1: Waislam**

Viongozi wa BAKWATA wanatakiwa wawe ni Waisilam. Sifa hii ndiyo inabeba MOYO halisi ya baraza. Kujitambua kuwa kiongozi anatakiwa kuwa muisilamu si kwa maneno, bali ni kwa kuitamka shahada kwa ulimi, kuitikadi kwa moyo na kasha kuendea mambo halisi ya vitendo.

**TAFAKURI**




1. ***Je, USILAM ni nini?***
2. ***Je, Muisilamu ni nani?***
3. ***Je, ni zipi nguzo za imaan zinazomfanya muisilam aitwe muisilam akizifuata?***
4. ***Je, ni zipi za Uisilam?***

Nina mnukuu Mwenyekiti wa Halmashauri kuu ya BAKWATA TAIFA, Sheikh Khamisi Mataka katika moja ya semina elekezi iliyofanyika BAGAMOYO tarehe 28 hadi 29/01/2022. Sheikh Mataka alisema;

‟ Hapana budi viongozi wa BAKWATA kujifunza Uisilam, maana hata maswahaba wapo waliojifunza Uisilam wakiwa ni watu wazima. Hii ndiyo hali ya baadhi ya viongozi wa BAKWATA, hata ule uisilam wenyewe hawaujui. Tusione aibu kujifunza kwa kuwa wapo maswahaba nao walijifunza wakiwa ni watu wazima.”

***Nukuu hapo juu ni dondoo fupi lakini kwa mapana sana darasa ile unaweza kulipata katika youtube kwa kutaipu semina ya Bagamoyo Sheikh Khamisi Mataka.***

**Sifa ya 2: Wanaume na Wanawake kwa wanawake wenzao.**

Hii ni sifa ya kimaumbile watu kujitambua kuwa ni ama mwaume au mwanamke na siyo maumbile yasiyotimia.

**Sifa ya 3: Baalegh**

Sifa hii inakamilisha maumbile ya mtu ambaye amepevuka. Maanake kama mtu hajapevuka hafai kupewa uongozi. Kwa msingi huu mtoto mdogo hatarajiwi kupewa uongozi mpaka anapofikia umri wa kupevuka na imethibiti kuwa amepevuka.

**Sifa ya 4: Wasiwe wendawazimu**

Maanake lazima kiongozi awe ni mtu aliyetimia kiakili. Hana hali ya wehu hata chembe. Kudhihirika kwa wehu ni kuwepo kwa vitendo halisi visivyokuwa vya kiungwana au kuthibitika kwa vipimo vya daktari.

**Sifa ya 5: Wasiwe Mafaasiq**

Fasiq ni mtu ambaye asiyeaminiki. Ni muongo.

Maanake viongozi wa BAKWATA hawatakiwi kuwa na hali ya udanganyifu au uongo. Uongo ni kinyume cha ukweli. Uongo na ukweli haukai pamoja. Hivyo viongozi kama wanakuwa ni waisilam wa kweli lazima wataishi maisha ya kuepuka kuwa mafaasiq.

**Sifa ya 6: Wawe wacha-Mungu na Waadilifu**

Ucha-Mungu ni kufuata yale yote anayoamrisha Allah na kuyaacha yale ambayo anayakataza. Mtu mchamungu anathibitika kwa kauli zake na vitendo vyake halisi. Taswira ya mtu mcha Mungu inapelekea kuwepo pia kwa uadilifu.

**Sifa ya 7: Wawe wenye kuchunga murua**

Murua ni tabia njema. Mambo yote yaliyolekezwa katika dini yanatofaa kuwa ni tabia njema lazima kiongozi ajipambe nayo. Asichupe mipaka na kuwa na mambo maovu.

**Sifa ya 8:  Wawe wenye himma katika Dini**

Himma ni juhudi katika kufanya mambo ya dini. Kujituma huku kiongozi akitaraji kupata radhi za Allah. Hii siyo kazi nyepesi kama mtu hana elimu  sahihi na uchamungu katika moyo wake. Hivyo kiongozi lazima ajikague mara kwa mara nafsi yake na kuona maeneo ambayo hajakaa sawa na kujikosoa mwenyewe. Uchamungu

**Sifa ya 9: Wawe ni ahlu Sunna Waljama'a**

Ni akina nani hawa wanaoitwa ahlu Sunna Waljama’a?

Kwa ufafanuzi mfupi kuwa ahlu Sunna Waljama’a ni waisilamu wenye kuwafuata mmoja katika maimu wanne ambao ni Imam Shafii, Imam Maliki, Imam Abuhanifa na Imam Hambali.

**Sifa ya 10: Wawe ni wenye kuikubali, Katiba ya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania na miongozo yake.**

Hii ni sifa inabeba nidhamu ya kiongozi katika kutii. Kiongozi ambaye hajabeba imaan halisi ya Uisilam kwanza hata kabla ya kutazama katiba anatakiwa kujua msingi mkuu wa mafanikio katika kutii mamlaka. Kiongozi kama hajui katiba au hana katiba ni wazi kwa zaidi ya asilimia 98 atakuwa anapinga mambo kwa ujinga ambao pengine yanatokana na makundi ya watu waovu, hivyo anakosa kujua kuwa anapinga maswala yaliyomo katika katiba. Mfano kuna ngazi tano za uongozi katika baraza, kuanzia TAIFA, MKOA, WILAYA, KATA na MSIKITI. Katika inaagiza nini kwa ngazi hizi atika utii?

i. **NGAZI YA MSIKITI:** Inatakiwa kutii na kutekeleza maagizo ya ngazi ya kata na ngazi zote za juu

Chini ya uongozi wa kamati ya msikiti, utekelezaji wa maagizo kikatiba umeelekezwa katika ibara ya 15 kifungu cha 1 kama ifuatavyo;

Ibara ya 15: Kamati ya Msikiti itakuwa na mamlaka na madaraka yafuatayo:-

***Kifungu cha kwanza (1): Kutekeleza Maagizo na Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Msikiti, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa.***

ii. **NGAZI YA KATA:** Inatakiwa kutii na kutekeleza maagizo ya ngazi ya Wilaya na ngazi zote za juu ya wilaya

Katika ngazi ya kata kuna halmashauri ya kata ambayo inawajibika katika shughuli za maendeleo. Hivyo kikatiba inawajibika katika kutekeleza maagizo ya ngazi za juu.

**Ibara ya 23:** Halmashauri ya Kata itakuwa na Madaraka na Mamlaka yafuatayo:-

***Kifungu cha kwanza (1): Kutekeleza Maagizo na Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kata na vikao vilivyo juu yake.***

iii. **NGAZI YA WILAYA:** Inatakiwa kutii na kutekeleza maagizo ya ngazi ya Mkoa na ngazi ya juu ya mkoa

**Ibara ya 34.** Halmashauri ya Wilaya itakuwa na Mamlaka na Madaraka hayayafuatayo:

***Kifungu cha kwanza (1): Kutekeleza Maazimio na Maagizo ya Mkutano Mkuu wa Wilaya, na vikao vingine vya juu vya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania (BAKWATA).***

iv. **NGAZI YA MKOA:** Inatakiwa kutii na kutekeleza maagizo ya ngazi ya Taifa

Ibara ya 45: Halmashauri ya Mkoa itakuwa na mamlaka na madaraka haya yafuatayo;-

***Kifungu cha kwanza (1): Kutekeleza Maazimio na Maagizo ya Mkutano Mkuu wa Mkoa na vikao vingine vya juu vya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania(BAKWATA).***

v. **NGAZI YA TAIFA:** Inatakiwa kuwa kiongozi wa ngazi zote za chini. Kama ngazi ya TAIFA ikiwa na msimamo kamili na wenye udhibiti mkali , lazima ngazi za chini zitabadilika. Ngazi ya TAIFA hapana shaka ndipo pana kazi kubwa ya kujenga taswira nzima ya baraza.

### 3.3. SIFA ZA ZA JUMLA ZA KIONGOZI YOYOTE

**Sifa za kiongozi bora ni hizi zifuatazo**

**i. Huruma**

Kiongozi anatakiwa awe mnyenyekevu,mpole,mwenye huruma ambayehuwahurumia wale anaowaongoza na mwenye kuwapendelea lileanalolipendelea nafsi yake. Kiongozi anatakiwa

daima kuwa yeyeni mtumishi wa wale waliomuweka katika uongozi, awaheshimukama mtumishi anavyomuheshimu bwana wake. Wakati huo huo,kiongozi anatakiwa ajiweke katika nafasi ya ulezi ambayo hanabudi kuwahurumia wale anaowalea.

ii. **Uadilifu**

Kiongozi muadilifu ni yule anayechunga haki za watu anaowaongoza. Yeye ni mchunga na mgawaji wa haki. Hana budi kuhakikisha kuwa yeye mwenyewe hachukui haki zake mpakaahakikishe kuwa kila mtu amepata haki yake.

iii. **Subira**

Kiongozi anatakiwa awe mwenye subira, mvumilivu na mstahimilivu. Kiongozi atekeleze wajibu wake ipasavyo na asitarajie kupendwa na kufurahiwa na watu wote.

iv. **Uoni wa mbali**

Kiongozi ni lazima awe na mtazamo wa mbali, ajue anakoipeleka jamii yake na aweze kubuni program za kuifikisha jamii huko.

v. **Uwezo wa Kubuni Mipango**

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe na uwezo wa kubuni mipango inayotekelezeka na mbinu bora za kufikia yale anayoyaona mbele.

vi. **Uwezo wa Kuunganisha Nguvu Kazi**

Kiongozi anatakiwa awe na uwezo wa kuunganisha nguvu kazi na yale yote yanayohitajika kufanikisha.

vii. **Utegemezi kwa Mungu**

Kiongozi na wale anaowaongoza wawe na tabia ya kumtanguliza Mungu kwa kila walifanyalo kwa kumtegemeayeye na kuchunga maamrisho na makatazo yake.

viii. **Msimamo katika Kuendea Lengo**

Kiongozi anatakiwa awe na msimamo thabitikatika kuendea lengo na wala asisukumwe na maslahi binafsi iweya vitu au sifa. Kiongozi asiyeyumbishwa na maslahi binafsihujijengea mazingira ya kuaminika hivyo kupata watu wengi zaidi kwa kushirikiana.

ix. **Mwenye Kujiamini**

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe na uwezo wa kujengamazingira ambayo yatamruhusu kila mtu kutoa mawazo yake kwauhuru,hili haliwezi kupatikana iwapo kiongozi hajiamini.Kiongozi atajiamini iwapo atadumu katika Ucha-Mungu nauadilifu.

x. **Uwezo wa Kuainisha Matatizo na KuyatafutiaUfumbuzi**

Kiongozi ni lazima awe na uwezo wa kutambua matatizoyanayoikabili jamii yake. Hili ni muhimu kwa sababu kulitambuatatizo ni hatua muhimu sana katika kuendea utatuzi wake. Hatuahii huanza kwa kulifafanua tatizo.

xi. **Mwenye Kujali Muda**

Kiongozi anatakiwa awe anajali matumizi yamuda wake. Kila sekunde aitumie kwenye mambo yenye manufaakibinafsi na kijamii.

xii. **Mwenye Kulenga Matokeo**

Kiongozi hatakiwi kufanya mambo ili mradi tu anafanya. Kilaanalolifanya lazima awe na matarajio fulani. Hivyo kiongozilazima awe mdadisi juu ya yale anayolenga. Kabla hajafanyalazima ajiulize; tunataka kupata nini na je inawezekana? Ninimatokeo, gharama na udhaifu wake?

**xiii. Mwenye kutegemea umadhubuti wa mtu nakuepa mapungufu na udhaifu wake**

Kiongozi aliye bora hujaribu kadiri ya uwezo wake kuwaleawatu na kuendana nao ili kila mmoja atoe mchango wake kulinganana uwezo wake. Na katika kwenda nao huwanasihi na kuhakikishakuwa udhaifu wa kila mmoja wao hauwi kikwazo kwa shughuli.

**xiv. Mwenye kukamata mambo machache muhimuna kudumu nayo katika utekelezaji**

Kiongozi bora ni yule anayechagua mambo machachemuhimu ya msingi na kudumu nayo katika utekelezaji. Mambomuhimu anayoyachagua ni yale ya kistratejia (strategical) ambayoyatatupa msingi na njia ya kuendea lengo kuu.

## DIRA, DHAMIRA NA TUNU

### DIRA YA BAKWATA (VISION)

DIRA YA BAKWATA: ***"Kuwa taasisi ya mfano kwa kuunganisha Waislamu wote wa Tanzania kiroho na kuchangia uboreshaji wa maisha ya jamii yote kwa ujumla."***

- **DIRA ni nini katika taasisi?**

Dira ya taasisi ni maono mapana yanayoelekeza taasisi inapotakiwa kuwa katika muda fulani. Kwa dira hiyo hapo juu ya BAKWATA kila kiongozi kwanza ana wajibu wa kuijua , lakini pia kuhakikisha anatembea nayo kila hatua kwa juhudi zote kuhakikisha anatimiza kufikiwa kwa maono hayo. Mheshimiwa Mufti Abubakari Zubeir katika awamu yake hii ya uongozi amejipambanua sana katika kuwaunganisha waisilam wala hakuna mwenye shaka juu ya swala hili. Kauli zake ambazo zimekuwa chachu kubwa zinachochea sana kila mkoa kuhakikisha kuna kuwepo na miradi ya kiuchumi ambayo itaboresha maisha jamii kwa ujumla. Ni wajibu wa lazima kila ngazi ya uogozi kujipambanua na namna wanavyoweza kutekeleza dira hii.

- NGAZI YA MSIKITI: Imam wa msikiti anawaunganisha vipi waisilam wa msikiti wake kwa kushirikiana na kamati yake ya msikiti ?
- NGAZI YA KATA: Sheikh wa kata anawaunganisha vipi waisilam wa kata yake kwa kushirikiana na Baraza lake la masheikh na Halmashauri ya kata?
- NGAZI YA WILAYA: Sheikh wa Wilaya anawaunganisha vipi waisilam wa wilaya yake kwa kushirikiana na Baraza lake la masheikh na Halmashauri yake ya wilaya?
- NGAZI YA MKOA: Sheikh wa Mkoa anawaunganisha vipi waisilam wa mkoa wake kwa kushirikiana na Baraza lake la masheikh na Halmashauri yake ya Mkoa?
- NGAZI YA TAIFA: Mheshimiwa MUFTI , ni mfano wa kuigwa kwa kuwaunganisha waisilam wa Tanzania leo, akishirikiana na Baraza la Ulamaa, Halmashauri Kuu, Bodi ya wadhamini, tume ya dini. Mfano huu ushuke ngazi za chini ili dira hii iweze kutimia kwa wepesi.

Maanake ni kuwa kama kila kiongozi katika eneo lake atatambua dira hii ndiyo maono ya BAKWATA halisi lazima sasa aweze kutoka katika mtazamo hasi na kurejea kwenye mtazamo sahihi. UMOJA NI NGUVU na UTENGANO NI UDHAIFU.
Kuwaunganisha waisilam ni swala la lazima au hiyari? Kwa kiongozi mwenye fikra nzuri lazima arejee historia ya Uisilam katika kujenga hoja zake.

Dira hii ya BAKWATA inatoa mafundisho halisi kutoka katika qur an tukufu katika Surat Aali Imraan aya ya 103, ambayo tafsiri yake ni;

***"Na shikamaneni kwa kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja , wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu…….."***

**DHAMIRA YA BAKWATA(MISSION)**

DHAMIRA YA BAKWATA : ***"Kueleza uelewa sahihi wa uislamu kulingana na misingi ya Qur'an, sunna na sheria nyingine mpya zinazoendelea katika uislamu kwa wa Tanzania wote. Ni matumaini yetu, inshaallah Bakwata itawezesha waislamu wote kuelewa dunia na maisha baada ya kifo."***

- Dhamira katika taasis ni nini?

Dhamira ni njia ya kuelekea kutekeleza DIRA ya taasisi.

Kwa dhamira ya maandishi hapo juu, kama kiongozi wa BAKWATA hajui dhamira ya BAKWATA ni vigumu sana kuiendea DIRA. Kwa mtu mmoja mmoja na kikundi cha watu katika umoja wao wanatakiwa kujikita sana katika kutathmini namna DHAMIRA zao moyoni zilivyo wakiwa ni viongozi ndani ya BAKWATA wakilinganisha na DHAMIRA hii kuu ambayo ipo kwa mujibu wa taasisi.
Je, ni kweli kama kiongozi katika eneo lake anaeleza watu kulingana na uelewa sahihi wa uisilam kulingana na misingi ya Qur an na sunna?
Kwa kuwa mwanya wa kujifunza uisilam bado upo kutokana na kuwa na uhai, hapana budi kiongozi ajibidiishe sana kuusoma uisilam na kueleza kwa ufahamu sahihi wa QUR AN na Sunnah.

**TUNU ZETU BARAZA (OUR CORE VALUES)**

Tunu katika taasisi ni nini?
Msomaji wa moduli hii, kwa ufupi tunu ni maadili (ethics) anayotakiwa kujipamba nayo kila mwanataasisi. Kwa hali hii taasisi inapokuwa imeandika tunu zake lazima zifundishwe katika taasisi na kila mwanataasis kujimbana nazo. Tunu hizi zinajenga DHAMIRA ya dhati kwa wanataasisi na hatimaye kufikia DIRA kuu.

Zifuatazo ndiyo tunu za BAKWATA;

i. Kuheshimu Qur'an Takatifu na Sunna za Mtume Muhammad(S.A.W).
ii. Sheria nyingine mpya kama mwongozo wa kufuatwaa na waislamu wote.
iii. Muhammad (S.A.W) ni mtume wa mwisho wa Allah.
iv. Uaminifu kwa jamii.
v. Uwajibikaji
vi. Kuheshimu haki za binadamu.
vii. Umoja ni nguzo muhimu ktk maendeleo.

viii. Thamani ya kupima UBORA (Quality) dhidi ya WINGI (Quantity)

**UCHAMBUZI WA KINA JUU YA TUNU ZA BAKWATA.**

i. Kuheshimu Qur'an Takatifu na Sunna za Mtume Muhammad(S.A.W).

Hii maanake ni kuwa kiongozi yeyote lazima aweke juhudi kubwa sana katika kuusoma uisilam kwa mapana yake na kisha kuheshimu kwa dhati qur an na sunna za mtume Muhammad(S.A.W). Kusoma kwa dhati uisilam kwa viongozi kunaleta tija kubwa kwao kuhakikisha uisilam unakuwa maisha ya jamii wanayoiongoza. Kinyume chake kama kiongozi hajasoma vyema uisilam matarajio ataongoza kwa utashi wake binafsi.

ii. Sheria nyingine mpya kama mwongozo wa kufuatwaa na waislamu wote.

Katika Bakwata kuna ngazi mbali mbali za uongozi (Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata, Msikiti). Kuna miongozo mbali mbali inatolewa, kuna maazimio mbali mbali yanatolewa, je wanaoongoza ndani yake wanafuata miongozo hiyo? Mfano kama maazimio ya vikao vya halmashauri kuu ya Taifa, maamizio ya mkutano mkuu wa Taifa n.k. Kutothamini miongozo na maazimio ni kuelekea kushindwa kufaulu. Hakuna mahala popote duniani utakuta kuna mafanikio ya taasisi au umma kama hawafuati yale ambayo yametolewa kama maamizio au miongozo inayostahili kufuatwa. Mabadiliko ya kiongozi wa BAKWATA leo hayatakuja kama ndoto za kulala na kuamka. Lakini mioyo ya nidhamu ijenge katika kuhakikisha wanafuata miongozo na maazimio yanayopitishwa.

iii. Muhammad (S.A.W) ni mtume wa mwisho wa Allah.

Tunu hii ni ya kiimani. Kutokana na upana wa maswala ya kiroho, kiongozi wa BAKWATA asichupe mipaka kuhusu swala la kuamini kuwa Mtume Muhammad(S.A.W) ndiyo mtume wa mwisho. Iwapo kuna kiongozi anakuwa na imaan nje yah ii lazima hastahili kamwe kuwa kiongozi kwa sifa.

iv. Uaminifu kwa jamii.

Hii ni tunu yenye tija kubwa katika jamii ambayo kwa kiasi kikubwa imepotea katika viongozi waliokuwa wengi ndani ya BAKWATA. Kulijenga baraza kuwa jipya na kasi kubwa ya maendeleo kupatikana ni kuhakikisha kuwa kila kiongozi anajipamba na sifa hii. Kama ambavyo inatakiwa mabadiliko yanaanzia katika nafsi ya mja mwenyewe kama ambavyo tayari Allah katoa maelekezo yake katika QUR AN aya ya 11 ya Surat Ra'ad (13) isemayo:

***"……..Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo naf-sini mwao………"***

v. Uwajibikaji

Uwajibikaji ni kinyume cha UVIVU au DHARAU. Kiongozi wa BAKWATA anatakiwa kuwa mtu mchapa kazi wa usiku na mchana huku akitarajia kupata radhi la Allah. Asitarajie kuwa

atakuwa na wepesi wakati anatimiza malengo yake. Lazima atakumbana na misuko suko mbali mbali kutoka kwa viongozi wenzake. Lazima ajikaribishe sana kwa Allah kwa dua mbali mbali na ibada zenye kumkinga na uhasidi. UWAJIBIKA ni zao la kujituma kutoka moyoni. Kama moyo ni mchafu lazima kiongozi atakwama kuwajibika ipasavyo. Hivyo lazima kiongozi asafishe moyo wake kwa kufanya amali njema ndipo atapa moyo halisi wa kuwajibika. Bila kuwa na moyo safi uwajibikaji hauwezi kusimama vyema.

vi. Kuheshimu haki za binadamu.

Hii ni tunu ambayo kama muisilam kiongozi hajausoma uisilam wake vyema inaweza kuwa vigumu sana kuheshimu haki za binadamu wenzake. Binadamu yeyote ni zaidi ya muisilam. Binadamu aliyetajwa hapa ni mtu yoyote. Kama tunu hii inamtaka kiongozi ndani ya BAKWATA kujipamba nayo, kila kiongozi anatakiwa kujitafakari kwa kina kuhusu mahusiano yake binafsi na kiongozi mwenzake ndani ya BAKWATA kisha ajitafakari kwa upana zaidi kuhusu kuheshimu haki za binadamu wengine. Kama ana moyo mbaya wa chuki na hasadi, ni wakati muafaka kujisahihisha kwa mafundisho ya moduli hii kuweza kukaa katika msimamo sahihi.

vii. Umoja ni nguzo muhimu katika maendeleo.

Anguko kubwa katika tunu hii. Kujitenga kumeleta udhaifu mkubwa sana. Katika kulijenga baraza kuwa imara sana katika maendeleo hakuna njia ya mkato lazima kuujenga umoja. Umoja katika ngazi ya msikiti, Umoja katika ngazi ya kata, Umoja katika ngazi ya Wilaya, Umoja katika ngazi ya Mkoa na UMOJA MKUBWA WA KITAIFA. Hakuna umoja ulioshindwa kufikia mafanikio kama kuna kujitambua kuwa umoja huo ni kwa ajili ya Allah. Waliotakasika katika nafsi zao baadhi ya maeneo wameanza kuweka umoja katika matendo na mafanikio yameanza kuchipuka.

Mfano Waisilam wa mkoa wa KAGERA na Mwanza wameweka mipango ya kujenga vituo vya afya katika kila wilaya. Ujenzi huu unakwenda kwa hali ambayo ndiyo mwendo wa umoja unatakiwa kuingia akilini. Hata kama kuna changamoto za hapa na pale za kufikia malengo lakini mikoa hii ndiyo kiigizo cha kuonyesha nguvu ya umoja katika kutuletea maendeleo ya kuujenga uisilam na jamii kwa ujumla. Hatua ambayo mikoa hii imefikia katika ujenzi wa vituo vya afya ni mfano mkubwa wa kuigwa Tanzania. Kwa bahati nzuri sana kila mkoa umekuwa unafanya kuwashirikisha wadau mbali mbali katika harambee za ujenzi bila kujali dini zao. Bado kuna waisilam ambao hawajawiva katika dhana hii ya umoja katika maeneo haya ya mikoa hii, lakini wanaona mabadiliko kila kukicha.

viii. Thamani ya kupima UBORA (Quality) dhidi ya WINGI (Quantity)

Kiongozi wa BAKWATA katika tunu hii lazima kila anachofanya azingatie ubora zaidi ya wingi. Katika tunu hii kila kinachofanyika kinatakiwa kuhakikisha kimezingatia ubora wa hali ya juu. Mfano kama wapo watu wachache wenye mioyo safi katika msikiti au wilaya au mkoa, hao watapiga hatua kubwa sana kwa haraka kuliko watu walio wengi ambao hawana usafi wa mioyo yao. Kujiletea maendeleo lazima kuzingatiwe sana swala la ubora. Ubora unatangenezwaje? Anza nafsi yako. Kisha mwambie na mwenzio, kisha na mwingine. Mkifika

watu 10, 20 au 30 mlio bora lazima mtalishinda genge kubwa la watu 100 ambao wamechafuka. Haukumbuki makundi makubwa mangapi yameshindwa na makundi madogo katika ufanisi. Haya makundi madogo kwa wingi wa watu yalikuwa bora sana kwa thamani kutokana na kutakasika kwa mioyo yao.

## BAKWATA NA MIPANGO

### UTANGULIZI

Lengo kuu la mada hii ni kuhakikisha kuwa katika ngazi mbali mbali za msonge wa uongozi wa BAKWATA , sasa waache kufanya kazi kwa mazoea na badala yake wajikite katika kuwa na mipango inayotekelezeka. Mazoea ya kufanya kazi bila kupanga pengine yametokana na kutojua thamani ya mipango. Mada hii itazindua kwa ufupi nadharia juu ya mipango kutokana na kazi kuu za uongozi na pia ushahidi wa kikatika ambao umeleekeza juu ya kupanga.

### NADHARIA YA KAZI ZA UONGOZI(MENEJIMENTI)


Wataalamu wa mambo ya menejimenti(Uongozi) wameelekeza kuwa kazi kubwa za menejimenti yoyote duniani ni nne ambazo ni;

i. KUPANGA (Planning )
ii. KURATIBU ( Organizing)
iii. KUONGOZA (Leading )
iv. KUDHIBITI (Controlling)

Kazi zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kupanga, kuratibu, kuongoza na kuthibiti rasilimali (Resources) ili kufikia MALENGO MAKUU ya taasisi.

Katika mgawanyo wa makundi, rasilimali zinawekwa katika makundi makuu matatu ambayo ni;

a) Rasilimali WATU (human Resources),
b) Rasilimali FEDHA( Financial Resource) na
c) Rasilimali Vitu (Physical Resources).



**MIPANGO NA USHAHIDI KUTOKA KATIBA YA BAKWATA**

Katika katiba ya BARAZA KUU LA WAISILAMU WA TANZANIA(BAKWATA) YA MWAKA 1999, toleo la mwaka 2018, neno **MIPANGO** limetajwa mara 13 katika IBARA zifutazo;

1. Ibara ya 9 kifungu cha 7.

Kinasomeka: Kusimamia, kuhimiza, kuimarisha, na au kusaidia kuweka MIPANGO ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa Zakka na Sadaka kwa kutimiza Amri ya Mwenyezi Mungu, na katika kuinua Dini na maendeleo ya Waislam.

2. Ibara ya 9 Kifungu cha 8.

Kinasomeka: Kusimamia, kuendesha, na au kusaidia kuendesha MIPANGO ya utunzaji na malezi kwa watoto yatima, watu wasiojiweza na masikini.

3. Ibara ya 9 Kifungu cha 10.

Kinasomeka: Kusimamia, kuhimiza, na au kuweka taratibu na MIPANGO ya 'Hijja na Umra' na huduma zake.

4. Ibara ya 10

Kinasomeka: Muundo waBaraza Kuu kwa utekelezaji wa **MIPANGO** na shughuli zake, Baraza kuu la Waislam wa Tanzania **(BAKWATA)** litakuwa na muundo huu ufuatao.

5. Ibara ya 23 Kifungu cha 2

Kinasomeka: Kushughulikia **MIPANGO** ya Daawa ya KatakwaWaislam wanaoishi katika eneola Kata husika.

6. Ibara ya 34 Kifungu cha 2

Kinasomeka: Kushughulikia **MIPANGO** ya Da'awa kwaWaislam wanaoishikatika Wilaya hiyo.
Msomaji wa moduli hii inabidi achukue katiba ya BAKWATA na kusoma ibara zilizobakia hapo chini.

7. Ibara ya 41 Kifungu cha 8.
8. Ibara ya 41 Kifungu cha 9.
9. Ibara ya 51 Kifungu cha 9.
10. Ibara ya 51 Kifungu cha 10.
11. Ibara ya 56 Kifungu cha 6(a)
12. Ibara ya 67 Kifungu cha 3
13. Ibara ya 83 Kifungu cha 3 kifungu kidogo cha 11.

Kurejewa kwa neno MIPANGO katika Ibara tofauti tofauti, kunachora taswira ya kuwa KIKATIBA, mipango inatambuliwa kuanzia ngazi ya TAIFA hadi ngazi ya chini kabisa ya MSIKITI. Kwa kuwa katiba inatambua swala la MIPANGO , hapana shaka kwamba kila ngazi inatakiwa kuwa na mipango mbali mbali katika maudhui mbali mbali.

## UPANGAJI WA MIPANGO

Kutokana na ulazima wa kazi za kiongozi yoyote katika ngazi yoyote ile na ushahidi wa kikatiba, hakuna budi sasa kila ngazi kutambua kuwa swala la upangaji wa mipango ni la lazima, hivyo lazima kujua pia kuwa wanapanga nini? Wanapanga kuwa na MPANGO MKAKATI wa miaka mingapi? Au kama bado hawajawa na weledi au watalaam wa mipango mikakati, je wanaweza kuwa na MPANGO KAZI? Mpango kazi wa mwaka, mpango kazi wa miezi mitatu au...?




## NAMNA YA KUPANGA

Kupanga ni taaluma kama zilivyo taaluma zingine. Si lazima watu wote wawe na taaluma hii, lakini ulazima ni kuwa kila kiongozi atambue kuwa na MPANGO ni lazima. Katika hali hii katika ngazi ya msikiti kuna kamati ya msikiti ambayo ndiyo jicho la msikiti, inaweza kuwatafuta miongoni mwa Waisilam wenye upeo mzuri wa kitaaluma na kuwaomba wasaidie katika kupanga mipango ambayo itawasilishwa katika kamati ya msikiti kisha kamati itachambua na kufikisha mbele ya waisilam katika mkutano mkuu wa msikiti.

Kupanga kwa kushirikisha makundi mbali mbali kuna faida kubwa ya mpango unaopangwa kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Huu ni muda wa kujitafakari kwa viongozi wa ngazi yoyote ile, kwamba wana mpango wa ngazi husika (kama ni msikiti, kata, wilaya, mkoa)? Si vyema kulalamika wakati fursa ya elimu imekufikia. Huu ni wakati wa kuamka na kufanya kazi.

# UTHUBUTU WA KUWEZA KATIKA MIPANGO

## UTANGULIZI

Lengo kuu la mada hii ni kuwaamsha viongozi ambao wanalalamika bila kuthubutu. Wanaweza wakadhani kwamba kulalamika kutafuta changamoto zinazowakabili Waisilam wanaowaongoza. Kumbe hakuna jambo la namna hiyo. Baadhi ya maeneo ndani ya uongozi wa BAKWATA wameamka mapema na kuacha kulalamika badala yake wakaanza kupanga mipango ya maendeleo na wanakwenda vyema. Hivyo kwa viongozi wa kutoka sehemu mbali mbali Tanzania, hawana budi kuamka na kuanza kufahamu kuwa swala la kupanga ni Kuthubutu na wala hakuna siku wataamka na kukuta Allah kawapatia maendeleo bila wao kupanga wanachotakiwa kufanya. Mada hii iwe chachu ya viongozi kujiweka sawa katika mipango yao ya maendeleo. Insha Allah hakuna mwanzo unakuwa mwepesi, lazima watakutana na changamoto na lazima wazikabili. Mabadiliko ya kutoka hali ya kuishi bila mipango na sasa wataona kuna mpango umekuja, lazima kuna changamoto watapitia na kuzikabili hizo changamoto ndiyo njia ya kufanikiwa unapatikana. Sasa ni wakati wa KUTHUBUTU. Je, kuna mifano ya waliothubutu katika kuweza walau hatua ya kwanza kupanga? Mifano ipo mingi na kwenye kuitafuta kuna baadhi ya mifano nitaitoa kama ya kujifunza (case study).

## MIFANO YA MIPANGO

Natambua kuwa ipo mipango mingi katika maeneo mengi, lakini kwa uchache nitoe mifano ya baadhi ya maeneo na kwa kupitia hii mifano sasa iwe ni chache kubwa kwa maeneo ambayo bado hayajathubutu kupanga.

### MSIKITI WA RAMWISHENYE- MKOANI KAGERA

Huu ni msikiti ambao upo katika wilaya ya Bukoba Mjini. Msikiti huu umekuwa ni wa mfano kwa kuthubutu kwake kuweka mpango wa kujenga msikiti wa kisasa wa ghorofa moja kwa kutumia swadaka la kila siku. Viongozi walikaa na kupanga kwa utulivu sana namna ya kuwa na uimara katika kukusanya swadaka la kila swala na kuweka mifumo bora kuthibiti matumizi ya fedha na kisha kuwa na uwazi wa matumizi ya fedha na hatimaye kwa miaka kadhaa sasa msikiti wa ghorofa moja umejengwa kwa thamani kubwa. Kwa kufuatilia kwa karibu sana mifumo bora ya uongozi wa msikiti huu, kumeweza leo kuandikwa kuwa ni miongoni mwa misikiti bora yenye kuthubutu kupanga na mpango ukafanikiwa.

## BAKWATA MKOA WA KAGERA

Uongozi wa BAKWATA mkoa wa Kagera katika moja ya historia iliyotikisa ndani ya Tanzania kwa mara ya kwanza ilijitokeza hadharani na kuzindua Mpango Mkakati wa maendeleo wa Miaka mitano (2019-2023). Ilikuwa tarehe 22/06/2019 ambapo mpango huu ulizinduliwa hadharani na mgeni rasmi akiwa ni Mkuu wa Mkoa Kagera kwa wakati huo alikuwa ni Brigedia Generali Marco Elisha Gaguti.

<table>
<tr><td colspan="2">KUZINDULIWA</td></tr>
<tr><td></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="2">Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Generali Marco Elisha Gaguti akiwa na viongozi wa BAKWATA wakati wa uzinduzi wa Mpango Mkakati wa Miaka mitano(2019-2023) tarehe 22/06/2019 katika viwanja vya Shule ya Nyashenye, iliyopo Bukoba Manispaa</td></tr>
</table>

Miaka mitatu sasa mpango mkakati unaendelea kutekelezwa. Pamoja na kuwa na vipaumbele vitano katika mpango mkakati huo, lakini kubwa zaidi linaloonekana kwa watu ni ujenzi wa vituo vya afya kila wilaya. Kuna jumla ya wilaya 8 na mpaka sasa moduli hii inapoandikwa vinajengwa vituo katika wilaya 6. Bado wilaya mbili zinajipanga na maswala ya ardhi.

## BAKWATA MKOA WA MWANZA

Uongozi wa BAKWATA MKOA wa Mwanza nao uko katika  ujenzi wa vituo vya afya katika kila Wilaya. Mpaka moduli hii inaandikwa tayari Wilaya nne kati ya saba zimeanza kujenga vituo vya afya kwa kutumia michango ya waisilam na wasiokuwa waisilam. Hii ni hatua kubwa katika kuendea mabadiliko halisi yakifikra ya kuwa na mpango wa maendeleo.

## MIKOA MINGINE

Ipo mikoa mingine ambayo imepanga kutekeleza mipango mbali mbali ya kilimo na uchumi na kazi zinaendelea. Muhimu sana kila mkoa sasa kuamka kuwa na ama mpango wa mkoa mzima ama mpango wa kila wilaya wa kuhakikisha kuwa wanakwenda mbele katika maendeleo.

## KUTHUBUTU KUPANGA

Bila shaka kama kiongozi amesoma moduli za kwanza za BAKWATA ONLINE ACADEMY za kozi ya Uongozi, Utawala Bora na TEHAMA, lazima atakuwa amepata kujua faida za kuwa na mipango. Zimefafanuliwa kwa kina katika moduli ya kwanza. Kama hajasoma moduli ile, sasa ni muda wa kuisoma. Kama alisoma na amesahau, huu ni muda wa kujikumbusha. Kuna faida gani za kuwa na mpango? Mpango mkakati ni jambo la kawaida na la kupuuzwa? Je kufanya kazi bila kuwa na mpango kuna maana gani?

| | |
|---|---|
|  | Alipata kusema Rais wa afrika ya kusini miaka mingi msemo wa kiingereza;<br><br>***"Action without vision is only passing time, Vision without action is merely dreaming, but vision with action can change the world"***<br><br>Fasiri ya maneno hayo katika lugha ya mipango;<br><br>***"Vitendo bila kuwa na mpango ni kupoteza muda, na Mpango bila kuwa na vitendo ni NDOTO, lakini mpango wenye vitendo unaweza kubadili ulimwengu"*** |

Ufafanuzi: Kwa nukuu hapo juu ya Nelson Maendela, maana yake ni kuwa MIPANGO yenye tija ni ile kwanza kabisa ILIYOPANGILIWA VYEMA(Vision), kisha ikaingizw y na kwenye VITENDO(Actions). Kuna tabia za kufanya mambo kwa zima moto bila kuwa na mipango. Lakini pia kuna tabia ya kupanga bila kutenda. Tabia hizi mbili muarobaini wake wa kuzitibu ni kuhakikisha kuwa sasa si wakati wa kutenda mambo bila kuwa na mipango, maanake itaishia patupu. Na kwa maana nyepesi sana watu wasije kuacha kupanga. Ushauri wa moduli hii ni kuwa kupanga walau kwa kuangalia wenzao wamewezaje kufanya mambo wakafanikiwa basi na wao wafanye juu chini kuhakikisha wanapanga kwa mazingira yao ili waweze kufanikiwa. Walau watoke wafanye ziara ya mafunzo kwa kuwatembelea wengine.

## CHANGAMOTO ZA MIPANGO NDANI YA BAKWATA

Waliothubutu kupanga mipango hawajakosa kukutana na changamoto ambazo kwa kupitia moduli hii lazima sasa kila wanaopanga katika msikiti, kata, Wilaya na Mkoa watambue watakutana nazo na hivyo wajijenge kwa dhati kuwa wao si wa kwanza katika kupata changamoto hizo na hivyo wasikate tamaa na rehema za Allah.

i. Wivu na chuki ndani ya viongozi wenyewe wa BAKWATA

Mpango mzuri wa msikiti au kata ukiwa umeletwa na kiongozi katika vikao halali vya BAKWATA, ukapokelewa vyema na wajumbe, wanatokea baadhi ya viongozi wenye wivu kuanza kuupiga vita na kuutengenezea propaganda chafu ukwame. Sababu za kina sana ni wivu wa kuona kiongozi mwenzao anapata umaarufu mkubwa bila kujali kwamba kuna maslahi makubwa ya jamii.

ii. Fikra za uoga

Baadhi ya viongozi wamekumbwa na fikra za kuogopa kusimamia mipango wanayopanga kwa kutokujiamini kwao kwamba wanaweza na kuweza kwao wanatakiwa kusimama zaidi na Allah na siyo vinginevyo.

iii. Utii na nidhamu

Kukosekana kwa utii na nidhamu imekuwa ni changamoto kubwa katika kufanikisha mipango ya maendeleo wanayopanga waisilamu wa maeneo husika. Mfano kama kuna kipaumbele cha wilaya nzima kinachohitaji michango ya kila msikiti, unakuta msikiti unakuwa na mgomo wa kuchangia. Hii inatokana na sababu nyingi ndani yake ikiwemo maadui wa uisilam (wanafiq) kuwa wamejipenyeza ndani ya BAKWATA kwa sura kama viongozi wa BAKWATA lakini kumbe ni wapingaji wa shughuli za BAKWATA moja kwa moja. Hii inaua kabisa ile methali ya UMOJA NI NGUVU na UTENGANO NI UDHAIFU.

Jambo lililohitaji nguvu ya pamoja kwa muda mfupi na kumalizika linachelewa na kusababisha manufaa ya umma kushindwa kutimia.

iv. Ujinga

Wapo watu wamshindwa kushiriki vyema mipango inayopangwa katika misikiti, kata, wilaya, mkoa si kwa sababu ya kiburi au unafiq wao, bali wengine ni wajinga wasiofahamu umuhimu wa mipango hiyo. Ujinga siyo tusi bali ni hali ya kutofahamu jambo fulani kwa wakati fulani. Wengine baada ya kuelimishwa kwa kina wanaweza kubadilika na kushiriki vyema. Hii imetokea kwa baadhi ya mipango.

v. Kukoseakana kwa vikao vya kutathmini mipango
Kupanga ni jambo jema, lakini kukosekana kwa vikao makini vya kutathmini ni tatizo kubwa sana. Rejea kanuni nne za menejimenti.

**UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MIPANGO**

Changamoto karibu zote hapo juu ambazo zimetajwa kama mifano michache katika mingi ambazo zipo ukizichambua ni kuwepo kwa MARADHI YA MOYO. Maradhi ya moyo ni kufa kwa moyo kwa kiongozi kwa maana kuwa na uchamungu hafifu hata kama ni msomi mkubwa wa dini au kuwa na dalili zote kuwa katika kundi la wanafiq(wanaodhihirisha uisilam na huku si muisilam kwa yakini ya moyoni). Hivyo katika mfumo mzuri wa BAKWATA kuanzia ngazi ya msikiti mpakaTaifa kuna chomo cha KIROHO kinachoshughulika na maswala haya ya kuhakikisha kuwa **WAUMINI NA VIONGOZI** wanakuwa katika hali safi kwa mafundisho ya kiroho. Kama inavyofahamika kwamba ROHO ikifa, basi mwili hauna kazi.

Vyombo hivi ni;

a) Ngazi ya msikiti: Kamati ya MSIKITI .
    - Kama inavyosomeka katika ibara ya 15 ya katiba ya BAKWARA kifungu cha 3.
b) Ngazi ya kata: Baraza la masheikh la kata
    - Kama inavyosomeka katika ibara ya 26 kuanzia kifungu cha 1 hadi 7.
c) Ngazi ya wilaya: Baraza la masheikh la KATA
    - Kama inavyosomeka katika ibara ya 37 kuanzia kifungu cha 1 hadi 7.
d) Ngazi ya Mkoa: Baraza la masheikh la MKOA
    - Kama inavyosomeka katika ibara ya 48 kuanzia kifungu cha 1 hadi 7.
e) Ngazi ya Taifa: BARAZA LA ULAMAA
    - Kama inavyosomeka katika ibara ya 62 kuanzia kifungu cha 1 hadi 15.

| **Na.** | **changamoto** | **Pendekezo la utatuzi** |
|---|---|---|
| i. | Wivu na chuki ndani ya viongozi wenyewe wa BAKWATA | Kutibu maradhi ya moyo kwa kufanya toba na kuwa wachamungu |
| ii. | Fikra za uoga | Kuafanya semina za mara kwa mara za ndani kwa ajili ya kujenga uwezo na kupanua fikra. |
| iii. | Utii na nidhamu | Kufanya semina za ndani za mara kwa mara na kutunga kanuni za uwajibikaji |
| iv. | Ujinga | Kufanya semina za ndani za mara kwa mara |
| v. | Kukoseakana kwa vikao vya kutathmini mipango | Vikao vya tathimini viandaliwe na timu za kitalaam |

| **TAKAFURI** |
|---|
| **Je, msikiti wako una mpango wa maendeleo wa Waisilam?** <br> **Je, kata yako ina mpango wa maendeleo wa Waisilam?** <br> **Je, katika wilaya yako au mkoa wako mna mpango wa maendeleo ya Waisilam?** <br> **Je, wewe ni mmoja wa viongozi wanakwamisha mipango au ni mmoja wanaotafuta pepo kwa kuunga mkono Mipango ya eneo lako?** |

Tanbih;

i. Baada ya kusoma moduli hii, kama viongozi wa msikiti au kata au wilaya au mkoa, hakikisheni mnaweka mipango madhubuti ya maendeleo ya waisilam na jamii kwa ujumla.
ii. Kama ngazi za juu hazina mwamko wa kuweka mipango anzeni katika ngazi ya msikiti wenu hapo hapo.
iii. Mpango wa maendeleo siyo lazima uwe na andiko kubwa wala ufundi mwingi, ni maswala ambayo kwa nguvu zilizopo ziwafanye waisilam wa ngazi ya msikiti au kata wajisikie wana uongozi wenye maarifa na uongozi umewaletea mipango ya kuwapeleka mbele.
iv. Katika kila mpango lazima maswala ya kumtanguliza Allah yawe na kipaumbele kwanza



## NIDHAMU NDANI YA BAKWATA

### UTANGULIZI

Swala la nidhamu ni swala la UCHAMUNGU. Kiongozi mwenye khofu ya kweli ya Allah katika moyo wake lazima atakuwa na nidhamu ya hali ya juu kwanza kwa Allah, kisha nidhamu ya viongozi wenzake ama wa juu ama wa chini yake. Ni swala la mtu mmoja mmoja kama kiongozi kujipima kiwango chake binafsi cha uchamungu kwa kuanzia na nidhamu anayoifanya ndani ya BAKWATA. Kama kiongozi anafanya kupuuza maelekezo, maagizo na ushauri wa viongozi wenzake ama viongozi wa juu yake, hapana shaka nidhamu yake iko chini au hana kabisa nidhamu.

## NIDHAMU KWA MJIBU WA QUR AN  NA SUNNAH

Kiongozi kukosa nidhamu au kuwa na nidhamu ya uoga, maanake ni kukosa kutambua juu ya mafundisho ya uisilamu au kuyajua na kuyapuuza.

Nukuu ya kutoka tafsiri ya aya ya 59 ya surat An-Nisa'

***Enyi milio amini, mtii Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume  na wenye mamlaka juu yenu, miongoni mwenu.***

## NIDHAMU YA KWA MUJIBU WA KATIBA YA BAKWATA




## NIDHAMU KWA VIONGOZI

Ni wajibu wa moja kwa moja kuwatii viongozi wa ngazi ya juu na wa ngazi za chini bila kupotoeza maana ya uchamungu wa mtu binafsi. Msomaji wa moduli hii hapa ni wajibu wako kusoma katiba ya BAKWATA na kutambua nafasi za viongozi mbali mbali waliotajwa katika katiba na kutambua nidhamu juu yao. Kiongozi mkuu ni Mheshimiwa Mufti.

## NIDHAMU YA NGAZI ZA JUU

**Nukuu kutoka Ibara ya 10. MUUNDO WABARAZA KUU**

Muundo wa Baraza Kuu kwa utekelezaji wa Mipango na shughuli zake, Baraza kuu la Waislam wa Tanzania **(BAKWATA)** litakuwa na muundo huu ufuatao:-

1. Ngazi ya Msikiti chini ya Uongozi wa Kata
2. Ngazi ya Kata chini ya Uongozi wa Wilaya
3. Ngazi ya Wilaya chini ya Uongozi wa Mkoa
4. Ngazi ya Mkoa chini ya uongozi wa Taifa
5. Ngazi ya Taifa.

**MAANA YAKE KATIKA KUZITAMBUA NGAZI HIZI, KILA NGAZI INA ULAZIMA KUTAMBUA KUWA UTII NI SEHEMU YA MAFANIKIO KATIKA TAASISI YOYOTE ILE**.

Mamlaka ya chini haipaswi kuhoji wala kudhihaki mamalaka ya juu inapokuwa imeagiza na badala yake inatakiwa kutekeleza. Hivyo vyema kujikumbusha kwa kunukuu katiba kama ifuatavyo;

**1. Ngazi ya msikiti**

Ibara ya 15 ya katiba katika kifungu cha kwanza; Kamati ya Msikiti itakuwa na mamlaka na madaraka yafuatayo:-

*"Kutekeleza Maagizo na Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Msikiti, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. "*

**2. Ngazi ya kata**

Kutoka katika Ibara ya 22 ya katiba; Halmashauri ya Kata itakuwa ndiyo chombo cha utekelezaji wa shughuli za Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania (BAKWATA) katika Kata, chini ya uongozi wa Mkutano Mkuu wa Kata.

Ibara ya 23 kifungu cha kwanza; Halmashauri ya Kata itakuwa na Madaraka na Mamlaka yafuatayo:-

*"Kutekeleza Maagizo na Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kata na vikao vilivyo juu yake"*


**3. Ngazi ya Wilaya**

Ibara ya 33. Halmashauri ya Wilaya itakuwa ndio chombo cha utekelezaji wa shughuli za kila siku za Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania (BAKWATA)katika Wilaya, chini ya Uongozi wa Mkutano Mkuu wa Wilaya.

Ibara ya 34 kifungu cha kwanza; Halmashauri ya Wilaya itakuwa na Mamlaka na Madaraka hayayafuatayo:

*"Kutekeleza Maazimio na Maagizo ya Mkutano Mkuu wa Wilaya, na vikao vingine vya juu vya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania (BAKWATA)."*

**TAFAKURI**




1. ***Je, bado unadhani kutii maagizo mamalaka ya juu ni hiayri?***
2. ***Je, kama viongozi wa msikiti mnakaa mnazingati kutii maagizo ya kata, wilaya, mkoa au Taifa?***
3. ***Je, kama viongozi wa kata mnapokaa mnazingatia kutii mamlaka ya wilaya, mkoa au Taifa?***
4. ***Je, unadhani utii unajengwa kwa kupewa adhabu au kwa kumcha***

***Allah?***

**MADHARA YA KUKOSEKANA KWA NIDHAMU**

i. Kukosa radhi za Allah (S.W).

Nukuu ya kutoka tafsiri ya aya ya 59 ya surat An-Nisa’

***Enyi milio amini, mtii Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu miongoni mwenu.***


ii. Kupata adhabu za maisha kwa mujibu wa mafundisho ya dini.

Hali duni ya maisha ya waliokuwa wengi inatokana na kumuasi Allah. Hii ni uthibitisho halisi wa kila kona kwa sababu ya utii kuwa mdogo au hakuna kabisa.

iii. Kushindwa kupata mafanikio kulingana na madhumuni ya kuanzishwa kwa BAKWATA au kufanya chini ya kiwango
iv. Kudharaulika kila kona ya nchi.
v. Kuzuka kwa migogoro inayovunja nguvu za maendeleo.

**NJIA ZA KUREJESHA NIDHAMU**

i. Kuwa wachamungu
ii. Kuwa na mikataba ya kazi/uongozi
iii. Kulipa haki za wafanya kazi
iv. Wafanyakazi kufanya wajibu wao kwa juhudi kubwa.
v. Kutoa pongezi kwa viongozi wanaofanya kazi vizuri
vi. Kufukuza viongozi wanaokiuka maelekezo kwa kiburi.



# MAANDALIZI YA VIONGOZI KUPITIA DAARUL MAARIF

## UTANGULIZI

Juhudi kubwa imeanza tangu mwaka 2016 ya kutafakari upya **MFUMO BORA WA KUANDAA VIONGOZI WA BAADAYE WA NDANI YA BARAZA**. Juhudi hii imeanza kwa kutafakari kuwepo kwa vyuo maalumu (DARUL MA'ARIF ) vya kuandaa viongozi ambavyo vitafundisha maarifa ya kina.

***Hatimaye Mhe. Mufti alimualika Rais mstaafu wa awamu ya pili mhe. Ali Hassan Mwinyi kufungua rasmi Daarul maarif. Mara tu baada ya swala ya Idil Adh-ha mwezi wa Dhul hijja mwaka 1437 iliyoswaliwa kitaifa BAKWATA makao makuu. Sawa na Mwezi wa tisa mwaka 2016.***

Chuo cha kwanza cha Daarul Maarifa kimeanzishwa BAKWATA makao makuu wilayani Kinondoni jijini Dar es salaam na tayari kimeshaanza kutoa mafunzo ya dini ya kiislamu kwa vijana.

## AZIMIO LA KUANZISHA DARUL MA'ARIF

Kuanzisha DARUL MA'ARIF katika Mikoa limekuwa ni azimio la vikao vya ngazi za juu vya BAKWATA na kwa hali hii kilichopo kwa sasa ni kila mkoa kujitafakari kwa kina namna ya kuliendea azimio hili.

## TUFANYE NINI KUHUSU DARUL MA'ARIF

i. Kuendeleza vyuo vilivyokwisha anzishwa katika mikoa kwa kujenga miundo mbinu bora
ii. Kuanzisha vyuo vipya katika mikoa ambayo bado haijaanzisha
iii. Kuandaa na kusimamia mtaala wa aina moja utumiwe katika vyuo vyote nchi nzima. Mtaala wa masomo ya dini na masomo ya mazingira) (lugha ya kiingereza , uongozi, utawala, Tehama na ujasiria mali
iv. Kuweka mifumo ya teknlojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kujifunza katika hali ya kisasa.
v. Kuwapatia mafunzo maalumu waalimu wanaofundisha vyuo hivi.
vi. Kufanya ziara za mafunzo kwa wanavyuo katika kuongeza njia za kujifunza.



**Mfano wa moja ya darasa katika jengo la DAR UL MAARIF linavyotakiwa kuwa la kisasa katika miundo mbinu kwa kupata maarifa kwa TEHAMA**

## UCHAMBUZI WA KAULI MBIU YA JITAMBUE, BADILIKA, ACHA MAZOEA

### UTANGULIZI

Lengo kuu la mada hii ni kujenga uelewa katika kufahamu kwanza maana ya kauli mbiu, lakini pia kujua umuhimu wa kauli mbiu katika taasisi yoyote duniani. Tayari miaka sita sasa Mheshimiwa Mufti Abubakari Zuberi katika uongozi wake amekuja na kauli mbiu ya JITAMBUE, BADILKA , ACHA MAZOEA. Kauli mbiu hii imekuwa ni kuchocheo cha fikra za watu mbali mbali kukimbilia tafsiri za kuona wanafanya mabadiliko.

### MAANA YA KAULI MBIU NA UMUHIMU WAKE

#### MAANA YA KAULI MBIU

Kauli mbiu kwa lugha ya kiingereza inafahamika kama SLOGAN.

Faisiri ya neno slogan kutoka Cambridge dictionary inasema;

**SLOGAN; a short easily rembered phrase, especially one used to advertise an idea or product.**

**An advertising slogan, A campain slogan.**

TAFSIRI YA Kiswahili;

Katika tafsiri isiyo ya moja kwa moja ni kuwa, KAULI MBIU ni sentensi fupi inayokuwa ni nyepesi kuimbuka na inayotumika kutangaza wazo au bidhaa.

Kauli mbiu hii ya JITAMBUE, BADILIKA, ACHA MAZOEA, ni wazi kwamba wazo kuu la Mheshimiwa Mufti ni kufanya mageuzi makubwa kupitia kujitambua,kubadilika na kuacha mazoea.

**UMUHIMU WA KAULI MBIU**

Kauli mbiu yoyote katika taasisi ina lengo la kuleta faida ya taasisi katika utendaji wake kwa;

i. Kuibadili taswira ya taasisi (brand)

Mitazamo ya watu katika kuiangalia taasisi inasemaje kwa wakati fulani na je taasisi inataka kuonekanaje katika jamii kwa wakati huo ili kuleta tija ya kufikia malengo yake?

ii. kuikuza bidhaa inayopatikana katika taasisi au huduma

Kwa muktadhwa wa BAKWATA ni taasisi inayotoa huduma kwa jamii. Kwa kuwa na kauli mbiu hii ni wazi kwamba nia ya kukuza mvuto katika kutoa huduma imeongezeka. Mfano wa huduma zinazotolewa na BAKWATA ni elimu kupitia shule za msingi, sekondari na vyuo vya kati,pia kusafirisha mahujaji na bila shaka katika sekta nyinginezo.

**UCHAMBUZI WA KAULI MBIU YA JITAMBUE, BADILIKA , ACHA MAZOEA**

BAKWATA kama taasisi inayohitaji kufikia malengo yake ya kikatiba na kuleta tija katika jamii, ilipokuja na kauli mbiu ya jitambue, badilika, acha mazoea, ilikuwa na malengo sambamba kama taasisi zote duniani zilinavyokusudia kauli mbiu iwavushe kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine.

**JITAMBUE**

KUJITAMBUA ni kujifahamu jinsi ulivyo kuhusiana na uwezo wako katika kuongoza, sifa nzuri na mbaya ulizonazo.

JITAMBUE: JE, una sifa nzuri na mbaya ? una karama zipi? una mapungufu yapi?

***Ukishajitambua, kiri mapungufu yako kwa wanafamilia yako au watu waliokaribu yako kwa kutumia sifa na uwezo wako kiakili, kimwili na kimaadili(kiroho) kufanikisha uongozi wako***.


Upana wa kujitambua kwa mwanadamu unaanzia katika kutambua kuwa yeye ameumbwa na Allah na amepewa majukumu maalum ya kufanya hapa duniani kwa muda na kasha ataondoka. Kwa taswira ya kiongozi linakuja swala la kujitambua kwake lazima kujitambua katika uwanja mpana wa uongozi wake. Ni upi uwezo wake wa kuongoza na upande upi ambao hana uwezo nao na afanye nini?

Kwa kiongozi mwenye kujitambua afanyi kila jambo pekee yake, bali anatafuta watu wenye maarifa husika wanafanya kwa ajili ya kuleta ufanisi. Hapana shaka kwamba Mheshimiwa Mufti kuja na kauli mbiu hii katika swala la KUJITAMBUA anamtaka kila kiongozi AJITAMBUE kwa maana ya ufafanuzi hapo juu. Kujitambua kwa kiongozi ni njia moja kwa moja atakuwa MWANGA katika jamii anayoongoza.

Katika mahafali ya kwanza ya wahitimu wa BAKWATA ONLINE ACADEMY iliyofanyika katika ukumbi wa Karimjee jiji Dar es Salaam tarehe 28/08/2022, aliyekuwa mgeni rasmi katika mahafali ile alikuwa ni Balozi wa Uturuki Nchini Tanzania, ambaye aliwaambia wahitimu wa kozi ya UONGOZI, UTAWALA BORA NA TEHAMA kuwa wao ni MWANGA wanaotakiwa kumulikia jamii.

Kiongozi anakuwa ni MWANGA kama anajitambua mapungufu yake na anatafuta namna ya kuyatatua matatizo hayo kwa kuunganisha vipaji vya watu wake.

**TAFAKURI**




1. ***Je, wewe unajitambua?***
2. ***Je, wewe unajitambua mapungufu yako?***
3. ***Je, katika kutambua mapungufu yako unajua njia za kutatua mapungufu yako?***
4. ***Je, baada ya kujitambua unaweza kuwazindua wenzako na wajitambue kama wewe?***

Uzoefu unaonyesha kila anayetamka kauli mbiu hii anasema kwa hamasa kubwa na kuonyesha wazi kuwa yeye sasa amejitambua na wenzake ndiyo bado hawajajitambua. Huu ni wakati wa kila mmoja kuzungumza na nafsi yake, ni kweli amejitambua? Njia zipi anazipitia katika kufikia kujitambua kwake ili alete tija?

**BADILIKA**

Mabadiliko ni kutoka katika hali mbaya kwenda katika hali nzuri. Haya yanaitwa mabadiliko CHANYA.

Mabadiliko ya kutoka katika hali nzuri kwenda hali mbaya ni mabadiliko HASI.

BADILIKA kama moja ya neno la kauli mbiu linachagiza kila mtu au kiongozi kutoka katika hali mbaya kwenda katika hali nzuri.

Mabadiliko yanaanzia katika nafsi ya mja mwenyewe kama ambavyo tayari Allah katoa maelekezo yake katika QUR AN aya ya 11 ya Surat Ra'ad (13) isemayo:

***"……..Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo naf-sini mwao………"***

Uzoefu unaonyesha kuwa kila mtu anapenda kulaumu mwenzake bila kujikagua yeye binafsi mapungufu yake kwanza. Kila mmoja anaojikagua na kujibaini mapungufu yake, kisha akabadili mwendo wake ndiyo mafanikio yake binafsi. Mafanikio yake binafsi yatajenga mnyororo mmoja na kupata watu wengi katika safu ya uongozi waliojikubali kubadilika kwako na ndiyo mafanikio yanapatikana. Hali mbaya ya utendaji katika ngazi mbali mbali ndani ya BAKWATA ni chanzo cha nafsi kutobadilika. Sasa weka dhamira ya kubadilika wewe binafsi na kisha weka azma ya mabadiliko yako kuwa sababu za kupata pepo kwa matendo yako.

### ACHA MAZOEA

ACHA ni katazo au kemeo la kufanya kitu.

Acha mazoea, bila shaka ni mazoea ya mambo mabaya. Mazoea ya kutenda mambo kwa kulipua lipua na kutokuwa na weledi nayo. Hii maanake ni kila jambo kiongozi analofanya ni lazima kujihakiki kuwa na ufahamu nalo. Kufanya kwa mazoea ya ukawaida na kudharau elimu ya jambo husika ni katika majanga ya kushindwa kwa kiongozi. Ukitaka kufanya vyema acha kufanya mambo kwa mazoea.

### MFUMO NA KAULI MBIU YA JITAMBUE, BADILIKA, ACHA MAZOEA

Kwa namna kauli mbiu ilivyotoka, unaweza kudhania kuwa inamgusa mtu binafsi tu. Kumbe upana wa kauli mbiu hii inatakiwa kwenda zaidi kutoka kwa mtu mmoja na kwenda KIMFUMO.

**MFUMO maanake ni nini?**

Neno jepesi ni kuwa MFUMO ni UTAWALA MZIMA. Maanake kwa lugha ya kiingereza kuwa ni SYSYTEM.

Mtu mmoja mmoja KAJITAMBUA, AMEANZA KUBADILIKA na AMEACHA MAZOEA, lakini MIFUMO ya utendaji nayo IMEJITAMBUA, IMEBADILIKA na KUACHA MAZOEA?

**MIFUMO**

Utajuwa kuwa mfumo upon a unafanya kazi kama mambo yafuatayo yanafanyika katika msikiti, kata, wilaya, mkoa au Taifa. Mifumo hii inakutambulisha kuwa sasa mifumo IMEJITAMBUA, IMEBADILIKA na KUACHA MAZOEA. Baadhi ya mifumo;

i. Kufanya kazi kwa mipango Mikakati
ii. Kufanya kazi kwa Mipango kazi na kalenda
iii. Kufanya vikao vinavyotakiwa kikatiba
iv. Kufanya vikao vyenye ubora kitaaluma
v. Kutekeleza maamizimo ya vikao
vi. Kuandaa kanuni na kuzisimamia utekelezaji wake

**Uchambuzi**

i. Kufanya kazi kwa mipango Mikakati

Swala kuwa na mpango mkakati si swala la hiyari kabisa katika taasisi. Kukosekana kwa mipango mikakati ni moja ya kuonyesha kuwa kauli mbiu bado haijaweza kutekelezwa KIMFUMO japokuwa mtu mmoja mmoja anajitambua kivyake vyake. Je, unadhani mipango ni jambo la kubahatisha? Kwanza tumeishasoma katika moduli hii juu ya kanuni nne za menejimenti. MFUMO usiopanga usitarajie kuwa MFUMO huo kupata matokeo kwa kubahatisha tu.

ii. Kufanya kazi kwa Mipango kazi na kalenda

Kutofanya kazi KIMFUMO ni kuwa na tabia ya kutopanga mpango kazi wala kalenda ya matukio. Inakuwa kama bendera fuata upepo.

iii. Kufanya vikao vinavyotakiwa kikatiba

Kufanya vikao ni swala la kuujenga mfumo sahihi wa kazi. Vipo vikao vya kikatiba ambavyo ni muhimu kufanyika na humo ndimo mambo ya taasisi yanajadiliwa. Kuogopa kufanaya vikao au kufanya vikao vya agenda za siri ni kuua mfumo na ni moja ya njia ya kutojitambua.

iv. Kufanya vikao vyenye ubora kitaaluma

Tayari mafunzo ya moduli ya kwanza ya Uongozi, Utawala Bora na Tehama imefafanua kwa kina mada ya mikutano na vikao. Kujitambua ni pamoja na kujitathmini vikao na ubora wake. Vingi katika vikao vinafanyika lakini havifuati kanuni za vikao hivyo na matokeo yake vikao vingi lakini tija hakuna.

v. Kutekeleza maamizimo ya vikao

Mfumo unajitambua lazima kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao. Kama hakuna utekelezaji wa maazimio ya vikao, basi hapo ujue mfumo umekufa na hakuna kujitambua.

vi. Kuandaa kanuni na kuzisimamia utekelezaji wake

Katiba haijitoshelezi kwa kila kitu, hivyo yafaa kuandaliwa kanuni za kuisadia katiba katika maeneo ambayo yana mapungufu.

# MALI ZA BAKWATA, UPOKEAJI WA WAQFU NA MATUMIZI YA WAQFU

## UTANGULIZI

BAKWATA ni moja nchi nzima. Kuna dhana potofu kwamba ngazi za uongozi kuwa zipo kitaifa, kimkoa, kiwilaya , kata na msikiti basi zipo BAKWATA nyingi. Hapana huo si ufahamu wa sawa sawa na umekuwa na upotoshaji mkubwa sana. Tunaposema BAKWATA ni moja maanake mali zake zote zinatakiwa kuwa chini ya chombo kimoja tu, amabcho ni bodi ya wadhamini. Hapa ifahamike vyema kuwa pamoja na kuwa mkoa au wilaya au kata au msikiti umeamua mfano kununua ardhi yake kwa matumizi yao, lakini lazima nyaraka kisheria zikamilishe mchakato wa kupata hati. Hati miliki halali inasainiwa na mwenyekiti wa bodi ya wadhamini. Mwenyekiti huyu ni mmoja tu kulingana na katiba. Mada hii inakusudiwa kujenga uwelewa wa pamoja wa mali za BAKWATA kisheria.

Pamoja na kufahamu dhana ya umiliki wa mali upo chini ya bodi ya wadhamini, kunabakia kuwa uendeshaji wa mali husika au usimamizi unabaki kuwa kwa mamlaka zili tafuta mali hiyo. Mfano ngazi ya msikiti wamepima kiwanja na kupata hati miliki ya kiwanja hicho kwa jina la BAKWATA, uendeshaji wa msikiti huo utabaki kuwa chini ya uongozi wa msikiti chini ya katiba ya BAKWATA.

## UFAHAMU KUHUSU BARAZA LA WADHAMINI

### UFAHAMU WA JUMLA

### MAANA YA BODI YA WADHAMINI

Bodi ya Wadhamini ni nini?

Maana yake ni Chombo chenye dhamana ya mali na fedha zote za jumuiya/taasisi

### KAZI ZA BODI YA WADHAMINI KWA UJUMLA

Taaluma ya uongozi duniani imefafanua kazi za bodi za wadhamini kwa ujumla katika taasisi nyingi zinafanana na zifuatazo ndizo kazi za bodi;

i. Kuweka DIRA, DHAMIRA na TUNU.
ii. Kuanzisha MPANGO MKAKATI (Strategic Plan).
iii. Kuanzisha na kufuatilia SERA (Policy).
iv. Kuhakikisha wanatunza nyaraka za umoja/taasisi mfano; Mikataba.
v. Kufuata sheria Inatakiwa kujua shuguli zote zinazofanywa ni halali.
vi. Kuhakikisha inaangalia sawa sawa Rasilimali za taasisi.
vii. Kuheshimu majukumu ya Wafanyakazi.
viii. Kuhakikisha uwajibikaji
ix. Kuhakikisha kama kuna mtumishi anaachishwa kazi, basi taratibu zinafuatwa.
x. Kuchagua , kusimamia majukumu ya mkurugenzi.
xi. Kuhakikisha utendaji imara.
    a. Kuitisha vikao vyenye faida.
    b. Kuunda kamati imara.

c. Shughuli za maendeleo
d. Kufanya mapitio ya utekelezaji katika vipindi maalumu.

xii. Kuitangaza jumuiya/taasisi

**UFAHAMU KUTOKA KATIKA KATIBA YA BAKWATA**

**Ibara ya 69. BARAZA LA WADHAMINI.**

Baraza la Wadhamini litakuwa na Wajumbe wafuatao:-
1. Wajumbe tisa (9) walioteuliwa na Baraza la Ulamaa.
2. Katibu Mkuu.

**Ibara ya 70.** Wadhamini watajulikana kwa jina la Wadhamini walioandikishwa wa Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania - **(BAKWATA) -*THE REGISTERED TRUSTEES OF BARAZA KUU LA WAISLAM WA TANZANIA (BAKWATA)***.

**Ibra ya 71.** Baraza la wadhamini litakuwa na uwezo wa kununua, kupokea, kuhamisha, kuweka rehani, kuuza na kusanifu kwa namna nyingine yoyote halali mali ya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania **(BAKWATA)** inayohamishika na isiyohamishika, baada ya kupata idhini ya Halmashauri Kuu ya Taifa na Baraza la Ulamaa.

**Ibara ya 72.** Baraza la Wadhamini litahakiki mali za Waqfu na kuziweka katika Hati Waqfu (Waqfu deed).

**Ibaya 73.** Baraza la Wadhamini litalinda na kuhakikisha kuwa Mali za Waqfu kwa namna yoyote ile haziuzwi.

**Ibara ya 74.** Baraza la Wadhamini litachagua Mwenyekiti wake kutokana na Wajumbe wake wenyewe.

**Ibara ya 75.** Kiwango cha kuweza kuendesha Mikutano ya Baraza la Wadhamini ni wajumbe watano.

**Ibara ya 76.** Itokeapo nafasi yoyote katika Baraza la Wadhamini, Baraza la Ulamaa litakuwa na uwezo wa kumteua Mtu atakayejaza nafasi hiyo hadi hapo Mkutano Mkuu utakapochagua tena Baraza la Wadhamini.

**Ibara ya 77.** Baraza la Wadhamini litakuwa na Muhuri maalum wa Nakiri (Seal) ambao utabandikwa juu ya Hati yoyote kumiliki au kuuza Mali na kutiwa saini na Wajumbe wa Baraza hilo, ili kuipa hati hiyo nguvu na uhalali. Pia muhuri wa Wadhamini utatumika katika hati yoyote ya kisheria inayohitaji Muhuri huo.

**Ibara ya 78.** Baraza la Wadhamini litakutana mara moja kwa mwaka, lakini linaweza kuitishwa na Mwenyekiti wake au Katibu Mkuu wa Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania **(BAKWATA)** au Baraza la Ulamaa.

## MALI YA BAKWATA

Mali ya BAKWATA inakuwa ni mali iliyokamilika kwa kutambulika kwakwe kisheria. Sheria inatambua nyaraka halali ambazo zinatambulika katika vyombo vya serikali. Mfano ununuzi wa ardhi lazima ufuate utaratibu wa kisheria na kukamilika kwa utaratibu huo ni kuwepo kwa nyaraka za umiliki ambazo mwisho lazima kuwepo na hati miliki ama kutoka kwa kamishna wa ardhi au hati ya kimila.

### WAQFU

### MAANA YA WAQFU

WAQFU kwa ufupi sana ni mali iliyotolewa kwa ajili ya Allah.

### Nani anayetoa waqfu?

Mtu yeyote ambaye anataka kupata radhi za Allah akiamua kutoa mali yake ifanye kazi kwa ajili ya kuendeleza Uisilam na kunufaisha jamii ya kiisilam.

Mtoaji huyu katika kutoa kwakwe waqfu anatarajia malipo yake kwa Allah yatakuwa ni endelevu hata kama akifa, bado thawabu zinaendelea kumfuata kadri mali inavyotumika (swadakat jaalia).

### Nani anayepokea?

Anayepokea waqfu ni mtu yeyote ambaye ameaminiwa kupokea kwa niaba ya waisilam. Mpokeaji hatakiwi kujimilikisha yeye mwenyewe, lazima ahakikishe kuwa mali ile inatumika kwa manufaa ya waisilam wote wanaotakiwa. Kutumia mali ya waqfu kwa manufaa binafsi ni makosa makubwa. Ni kula mali ya umma.

### WAQFU KATIKA BAKWATA

**Ibara ya 72.** Baraza la Wadhamini litahakiki mali za Waqfu na kuziweka katika Hati Waqfu (Waqfu deed).

**Ibaya 73.** Baraza la Wadhamini litalinda na kuhakikisha kuwa Mali za Waqfu kwa namna yoyote ile haziuzwi.

### UPOKEAJI WA MALI ZA WAQFU ZA BAKWATA

Kama maelezo hapo juu yalivyotangulia kufafanua kuwa mtu yeyote aliyeaminiwa katika eneo husika anaweza kupokea waqfu kwa niaba ya BAKWATA, lakini lazima akamilishe umiliki huo kwa kuwasilisha nyaraka kwa bodi ya wadhamini. Bodi ya wadhamini itaandaa Hati ya Waqfu (Waqfu deed).

**UZOEFU ULIOPO**

i. Ufahamu mdogo kuhusu uwasilishaji wa nyaraka za waqfu kwenye bodi.

Katika mikoa mbali mbali bado kuna upeo mdogo wa kufahamu maswala ya waqfu na kwa dhana ya BAKWATA pia nyaraka za waqfu kutoka mikoani hazifiki kwenye bodi kwa ajili ya kuandaa hati za waqfu.

ii. Ubinafsi.

Pamoja na ufahamu mdogo lakini wapo wanaofahamu kwa kina hatua zote za ukamilishaji wa taratibu wa waqfu kisheria, lakini wanaingiwa na ubinafsi katika mioyo yao kwa kuona kwamba zitakuwa ni mali za umma. Hivyo nafsi yenye ubinafsi inaamua kuweka mali hiyo kinyemela chini kwa chini kwa matumizi ya aidha mtu mmoja au kakikundi ka watu wachache kwa manufaa yao binafsi.

iii. Kibri na dharau za mamlaka

Kutokana na baadhi ya viongozi kutokuwa na ufahamu wa maswala ya umuhimu wakuwa na nidhamu ama kutokuwa na uchamungu, wanashindwa kukamilisha maswala ya

**KUREKEBISHA MAKOSA YALIYOPO**

i. Elimu

Elimu iendelee kutolewa kwa viongozi mbali mbali wanaosimamia kazi za BAKWATA

ii. kumcha Allah

Kumcha Allah ndiyo suluhisho la mambo yote. Kwa maana kama mtu hajui na ni mcha mungu atalazimika kuuliza kwa wanaojua kuliko kufanya makosa.

## MFANO WA MAANDISHI YA KUTOA WAQFU

### MAKUBALIANO YA KUTOA WAQFU

**MAKUBALIANO** haya yamefanyika leo ……**.** mwezi …………………**…**2022

**KATI YA**

ALLY JUMA RAMADHANI **wa sanduku la barua Na.** 456, **-**TABORA, **(ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "**MTOA WAQFU"**ikijumuisha warithi au wasimamizi )kwa upande mmoja;**

**NA**

JUMA RAMADHANI SAIDI **wa** S.L.P 36 **, -** TABORA **(ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "**MPOKEA WAQFU" **ikijumuisha msimamizi au muwakilishi wake)kwa upande wa pili kwa niaba ya BAKWATA.**

KWAMBA: MTOA WAQFU **ni mmiliki halali wa** kiwanja Na. 202**,** Kitalu Na. "A" **chenye ukubwa wa** mita za mraba 1000 **kilichopo eneo la** Ng'ambo **wilaya ya** TABORA MIJINI **katika mkoa wa** TABORA .

KWAMBA: MTOA WAQFU **ana nia ya kutaka kutoa kiwanja chake tajwa kwa njia ya** *wakfu* **kwa "**MPOKEA WAQFU" **kwa ajili ya kufanyia maendeleo ya waislam chini**.

KWAMBA: WAPOKEA WAQFU **watakuwa wasimamizi wa kuu wa kuhakikisha wa malengo na nia ya** MTOA WAQFU **yatatekelezwa kwa mujibu wa mkataba huu pasina kukiukwa.**

**NA KWAMBA: MTOA WAQFU** na **"WAPOKEA WAQFU**" wanakubaliana kwa pamoja kuzingatia na kuheshimu taratibu na masharti yaliyowekwa katika Mkataba huu;

KWA HIYO PANDE ZOTE MBILI WAMEKUBALIANA NA MKATABA HUU UNASHUHUDIA *ifuatavyo: -*

**1. <u>KUTOLEWA KWA WAQFU</u>:**

MTOA WAQFU **akiwa ni mtu mzima , mwenye akili timamu na mzima wa afya ya mwili, bila ya kushurutushiwa, kulazimishwa, kulaghaiwa, anatoa mali yake ambayo ni** kiwanja Na. 202**,** Kitalu Na. "A" **chenye ukubwa wa** mita za mraba 1000 **kilichopo eneo la** Ng'ambo **wilaya ya** TABORA MIJINI **katika mkoa wa** TABORA .

JUMA RAMADHANI SAIDI **wa** S.L.P 36 **, -** TABORA **( kama** WASIMAMIZI **wa mali hiyo ya Waqfu kwa niaba ya BAKWATA).**

2. **KUANZA KWA WAKFU**

   **MTOA WAQFU** anatoa moja kwa moja (permanently) kiwanja hicho kama wakfu kutoka leo tarehe ya kusainiwa makubaliano hayo na kiwanja kitaendelea kuwa mali ya waqfu na hakitorudi kwa **MTOA WAQFU**, wala warithi wake, wasimamizi wake wa mirathi au wakala wake.

3. **MADHUMUNI YA KUTOLEWA KWA WAQFU:**

**3.1.** MTOA WAQFU **anatoa kiwanja tajwa kwa ajili tu ya kufanya maendeleo ya dini ya kiislamu na waislamu tu. Mara baada yakuhamishwa umiliki wa mali ya waqfu , "**WAPOKEA WAQFU" **haruhusiwi kwa namna yeyote ile kubadili matumizi ya mali ya waqfu, ama kukiuza, kuweka reheni, kukigawa ( partition) au kwa namna yeyote ile haruhusiwi kubadili matumizi ya mali ya waqfu kutoka katika lengo la kutolewa kwa mali hiyo.**

**3.2.** **Fedha zote zitakazo toka na mali ya waqfu zitumike kwa ajili ya maendeleo ya uislamu na waislamu tu.**

4. KUTOKUJUMUISHWA KATIKA MALI ZA MIRATHI ZA MTOA WAQFU

   MTOA WAQFU **hatodai au kuijumuisha au warithi wake hawatodai au kuijumuisha mali ya waqfu kuwa ni moja ya mali za** MTOA WAQFU **katika kipindi chote cha uhai wake au baada ya kufikwa na umauti.**

5. **NGUVU ZA MAKUBALIANO:**

   Makubaliano haya yataanza kuwa na nguvu kisheria mara baada yakuwekwa sahihi na pande zote na hayatakuwa na kikomo wakati **MPOKEA WAQFU** amekwisha hamishiwa umiliki wa kiwanja alichokabidhiwa.

6. **KUKABIDHI NYARAKA ZA UMILIKI**

   **MTOA WAQFU** atawakabidhi **"WAPOKEA WAQFU"** nyaraka zote za umiliki wa kiwanja siku ya kusainiwa kwa makubaliano haya.

7. **UTHIBITISHO WA UMILIKI WA MTOA WAQFU:-**

**MTOA WAQFU** anathibitisha kuwa kiwanja anachotoa waqfu ni mali yake mwenyewe, si kiwanja cha familia au cha ukoo na kwamba hakuna madai ya mtu mwingine kuhusiana na umiliki wa kiwanja hicho na pia hakuna mgogoro wa mipaka eneo la kiwanja hicho, wala hakijawekwa rehani au kuwa na deni la aina yeyote.

8. **UHALALI WA MAELEZO YALIYOTOLEWA KABLA YA KUSAINI MAKUBALIANO HAYA**

9.1. **MTOA WAQFU** anathibitisha kuwa maelezo yote yaliyotolewa kabla ya kusaini Makubaliano haya ni ya kweli na kwamba hakulazimishwa au kushurutishwa kwa aina yeyote kutoa maelezo hayo ili kuingia katika makubaliano haya

9.2. Endapo mgogoro wowote utajitokeza kuhusiana na kiwanja kinachotolewa waqfu katika Mkataba huu baadaye, **MTOA WAQFU** anakubali kushirikiana katika kutatua mgogoro huu.

9. **UKAMILIFU WA MAKUBALIANO HAYA**

Makubaliano haya yatakuwa ni makubaliano kamili baina ya **MTOA WAQFU** na **"WAPOKEA WAQFU**" na hakuna makubaliano mengine au nyaraka nyingine yeyote iliyosainiwa baina ya pande mbili hizo itakayotumika au kutambulika kisheria kama makubaliano halali yanayohusiana na kutolewa waqfu kwa kiwanja tajwa.

10. **TAFSIRI YA MKATABA**

Mkataba huu utasomeka na kutafsiriwa kulingana na sheria za Mikataba zinazotumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA KUTHIBITISHA **haya yote yaliyotamkwa hapo juu, pande zote mbili wameweka sahihi zao, siku na tarehe zilizooneshwa hapa chini**

MTOA WAQFU
JINA KAMILI ……………………………………………..….
SAINI ……………………………………………..…..
ANWANI ……………………………………….….…..
WADHIFA ………………….…………………….……….…

SHAHIDI WA MTOA WAQFU
JINA KAMILI ……………………………………………..….

SAINI ……………………………………………..
ANWANI ……………………………………………..
WADHIFA ……………………………………………

IMEWEKWA SAHIHI na KUTOLEWA kwa niaba ya
**MPOKEA WAQFU**

**tarehe …………….. mwezi ……………….2022**

JINA KAMILI ………………………………………….
SAINI ……………………………………………..
ANWANI ……………………………………………..
WADHIFA ……………………………………………..

JINA KAMILI ………………………………………….
SAINI ……………………………………………..
ANWANI ……………………………………………..
WADHIFA ……………………………………………

MAKUBALIANO HAYA YAMETHIBITISHWA NA ( SERIKALI YA MTAA)
JINA KAMILI ………………………………………….
SAINI ……………………………………………..
ANWANI ……………………………………………..
WADHIFA ……………………………………………

UMESHUHUDIWA NA : ( WAKILI)

JINA KAMILI ………………………………………….
SAINI ……………………………………………..
ANWANI ……………………………………………..
WADHIFA ……………………………………………..

**Angalizo:**

i. Kwa kuwa uzoefu umeonyesha kuwa waqfu nyingi zinashindwa kuandikwa kwa usahihi, ni matarajio muongozo hapo juu utakuwa ni kielelezo cha mfano kuwaongoza wanaotoa na wanaopokea kwa niaba ya BAKWATA.
ii. Baada ya kupokea waqfu kwa niaba ya BAKWATA, utaratibu wa kufikisha nyaraka kwa katibu mkuu na hatimaye bodi ya wadhamini zifanyike ili kupata waqfu deed.

# UCHAMBUZI WA HALI YA BAKWATA (SWOT ANALYSIS).

## UTANGULIZI




Kila taasisi duniani inatakiwa kujifanyia uchambuzi wa hali halisi ambao kwa lugha ya kiingereza unafahamika kama SWOT analysis. Uchambuzi huu ni muhimu sana kujenga ustawi wa taasisi. Taasisi inapojifanyia uchambuzi huu inalenga katika kuangalia mazingira ya ndani ya taasisi (Internal Environment) na mazingira ya nje (External Enviroment). Kuangalia mazingira ya ndani na nje kunaleta faida kubwa sana katika taasisi kwa sababu ni wakati huo taasisi inataka kutumia vyema NGUVU NA FURSA zake katika kujiletea maendeleo na pia ni wakati huo taasisi inataka kujiondoa na UDHAIFU na kujikunga na MATISHIO/VIKWAZO. Hakuna wakati maendeleo ya taasisi yatakuja kwa watu kulalamika au kusukumiana mzigo bila kujua mambo ya msingi ya kuyaendea.

### Mazingira ya ndani (Internal Enviroment)

Mazingira ya ndani ya taasisi maanake ni mambo yote ambayo yapo ndani ya uwezo wa taasisi. Katika SWOT analysis, hapo huwa inachukuliwa SW.

Maana ya SW ni Stength (Nguvu) na Weakness(Udhaifu).

Kujua NGUVU zetu na FURSA zinazotuzunguka, kutatupa kujitathmini kwa kina tumetumia vyema nguvu zetu kwa manufaa ya kujiletea maendeleo? Au hatukujua kabla ya mpango na sasa tumejua, tutajenga ari mpya ya kuleta mabadiliko baada ya kumuomba Allah athibitishe matumizi ya nguvu zetu na fursa zinazotuzunguka kuwa sababu ya mafanikio.

### Mazingira ya nje (External Environment)

Katika uchambuzi wa mazingira ya nje maanake taasisi inajitathmini mambo ambayo yapo nje ya uwezo wake. Hapo katika SWOT analysisi tunachukua OT.

Maana ya OT ni Opportunity(Fursa) na Threats(Matishio).

Kujua pia FURSA zetu na MATISHIO yanayotuzunguka kutatupa mwanga wa kujua mikakati ya kutumia fursa na kukabiliana na matishio hayo kwa lengo la kuboresha na kuacha kulalama pasina kuchukua hatua stahiki?

## MAZINGIRA YA NDANI YA BAKWATA (NGUVU NA UDHAIFU)

## NGUVU ZA BARAZA (STRENGTHS)

Hizi ni baadhi ya NGUVU za baraza kwa uchambuzi wa moduli hii, ambazo zikitumika vyema zitafanya maendeleo kuwa ya hali ya juu sana.

i. Kuwepo katiba iliyosajiliwa.
ii. Kuwepo kwa mtandao/msonge wa uongozi kutoka Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata/Mtaa hadi Msikiti.
iii. Uwezo wa kujenga na kuendeleza misikiti, madrasa na daarl-maarif
iv. Uwezo wa kuratibu matukio ya hijja kutoka kimataifa na kitaifa.
v. BAKWATA kuwa na mahusiano mazuri na taasisi nyingine.
vi. Kuwepo kwa miongozo ya kina inayotokana na Qur an na Sunnah na sheria nyingine zinazotokana na uisilam.
vii. Kuwepo kwa majengo, ardhi, rasilimali watu na vitega uchumi vingine vinavyoingiza mapato.
viii. Kuwepo kwa MAJILIS TANSIQ kwa ajili ya kuratibu na kuweka uunganisho mzuri na taasisi/jumuiya zingine za kiisilam.
ix. Kuwepo kwa taasisi za elimu za kidini na kisekula zinazomilikiwa na BAKWATA.
x. Kuwepo kwa baraza lenye nguvu ya usuluhishi wa maswala ya ndoa za kiisilamu na maswala ya kijamii na kiuchumi kuanzia ngazi ya Msikiti, Wilaya , Mkoa hadi Taifa.

## UDHAIFU WA BARAZA (WEAKNESS)

Haya ni baadhi ya madhaifu, sasa ni jukumu letu kama msikiti, kama kata, kama wilaya, kama mkoa au Taifa kuamua kuyaondoa kwa kuchukua hatua stahiki. Kuna uwezekano kuwa ngazi moja ya uongozi ikaamua kukaa chini na kutafakari moja moja na wakaanza kuchukua hatua ya kuyaondoa kwa vitendo.

i. Ofisi za BAKWATA kutoendeshwa kwa weledi (professional).
ii. Katiba ya BAKWATA inakosa kuwa idara katika halmashauri ya mkoa na Wilaya na hivyo kufanya kukosekana kwa uwajibishaji watu kwa idara zao.
iii. Ukosefu wa fedha za kutosha kujiendesha na kujitegemea.
iv. Kutokuwa na hadidu za rejea za kutosha na majukumu ya kazi.
v. Kutokuwepo na utunzaji wa kumbu kumbu, nyaraka na mfumo wa taarifa wa kwa program, mipango na shughuli ndani ya BAKWATA na taasisi zilizo chini yake.

vi. Kutokuwepo kwa mipango, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini.
vii. Uchache wa kusambaza maarifa ya usilamu na kutokuwepo kwa programu za kujenga uwezo kwa viongozi na maafisa waajiriwa katika BAKWATA.
viii. Kukosekana kwa taarifa za fedha na mfumo wa kifedha.
ix. Kukosekana kwa kanuni za fedha.
x. Kukosekana kwa majukwaa (platform) kwa ajili ya kubadilishana taarifa.
xi. Kukosekana kwa usimamizi na uratibu kwa taasisi za chini ya BAKWATA.
xii. Kukosekana kwa utunzaji wa rasili mali (Assets) za BAKWATA.
xiii. Kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji katika uhamasihaji wa rasimali,kupanga rasilimali na matumizi ya rasilimali
xiv. Kukosekana kwa sera na miongozo kwa mageuzi mbali mbali ya kiroho na kiuchumi.
xv. Kukosekana kwa usajili na kanzi data kwa rasilimali za Waisilamu na madeni.
xvi. Katiba haijashirikishwa vyema kwa wadau.
xvii. Kutokuwepo kwa sera na miongozo mipya iliyoboreshwa kwa ajili ya mageuzi (interversions) ya kiuchumi na kijamii.

**MAZINGIRA YA NJE YA BAKWATA(FURSA NA TISHIO)**

**FURSA ZA BARAZA (OPPORTUNITIES)**

i. Kuwepo kwa umma mkubwa wa Waisilamu.
ii. Kuwepo kwa waisilamu wengi waliosoma elimu zote mbili (dini na sekula)
iii. Uhusiano mzuri kati ya BAKWATA , Serikali na taasisi zake, NGOs, CSOs na taasisi nyingine za kidini.
iv. Kuwepo kwa taasisi za kiisilam ambazo zinataka kushirikiana na BAKWATA katika kukamilisha malengo ya BAKWATA.
v. BAKWATA ni taasisi ina hadhi ya kukubalika na taasisi mbali mbali ikijumuisha Serikali, Taasisi zisizo za kiisilam.
vi. Mazingira ya amani ya Waisilam kufanya ibada zao za kiroho.
vii. Utayari wa wafadhili kuchangia katika maswala yanayohusu Ustawi wa Uisilamu.

### TISHIO/VIKWAZO KWA BARAZA (Threats/challenges)

i. Changamoto za kiroho kwa jamii ya vijana wa kiisilamu kutokana na kukosekana kwa miongozo ya malezi ya kiisilamu na mkumbo wa utandawazi.
ii. Kupungua kwa kiwango cha maarifa katika jamii ya kiisilamu ndani ya Tanzania.
iii. Kutegemea wafadhili.
iv. Ufahamu mdogo wa jamii ya kiisilamu katika lugha ya kiarabu na hivyo kupelekea mawasiliano duni katika kuleta mageuzi.

### MAJUKUMU YA KUFANYA UCHAMBUZI WA HALI BAKWATA (SWOT ANALYSIS).

Baada ya kusoma hapo juu mifano ya uchambuzi wa hali hali ya BAKWATA, sasa ni jukumu la MSIKITI, KATA, WILAYA AU MKOA kukaa kikao kazi na kufanya uchambuzi kama huo na kufanyia kazi. Kuweka muhtasari mzuri wa uchambuzi, kikao kazi kinaweza kuwa na jedwali kama hapo chini;

| **Mazingira ya ndani** | | **Mazingira ya nje** | |
|---|---|---|---|
| Uwezo/nguvu | udhaifu | Fursa | Vikwazo/Tishio |
| i. | i. | i. | i. |
| ii. | ii. | ii. | ii. |
| iii. | iii. | iii. | iii. |
| iv. | iv. | iv. | iv. |

## UCHUMI NDANI YA BAKWATA NA USIMAMIZI WA FEDHA

### UTANGULIZI

Katiba ya Bakwata imeweka madhumuni yanayoakisi masilahi ya Uislamu na Waislamu nchini kama yanavyobainishwa katika Ibara ya 9 (1-17). Yapo madhumuni 17. Kuhusu uchumi, katika katiba ibara ya 9 inaelekeza.
Ibara ya 9 kifungu cha 5 kinasema; **"Kuwahimiza na kuwasaidia Waislamu nchini kuanzisha miradi na shughuli za uchumi na uzalishaji mali kwa lengo la kuupiga vita umaskini"**

### a) KUHIMIZA NA KUSAIDIA

**KUHIMIZA** kuna njia mbali mbali zinazoweza kutumika kama hii **KUWASOMESHA (semina za ana kwa ana na mafunzo ya ONLINE) KUWASAIDIA** pia njia nyingi zinaweza kutumika katika kusaidia huko. Njia kubwa na ya kwanza kabisa ni kuwapa maarifa. Maarifa yamejificha katika elimu ya mfumo rasmi na mfumo usio rasmi. Upo msemo wa

Kiswahili kwamba **"Ukitaka kumsaidia mtu kupata samaki wa kula muda wowote ni kumfundisha kuvua samaki na siyo kumpa samaki".** Maana ya moja kwa moja hapo ni kumpa mtu MAARIFA ya jambo husika. Kumpa mtu maarifa kunampa nguvu kubwa ya kuendelea kutumia maarifa hayo muda mrefu kuongeza kipato chake kuliko kumpa fedha mara moja kisha muda mwingine akarudi kuwa omba omba.

## b) MIRADI, UCHUMI, UZALISHAJI MALI

Je, ufahamu wa neno mradi mpaka uwe na sifa zipi? Ufahamu wa neno UCHUMI nao uko vipi? Hali kadhalika uzalishaji mali tunafahamu nini na tunafanya nini mpaka sasa. Maswali haya yanajibika ndani ya moduli hii na ndiyo njia muafaka ambayo BAKWATA inakwenda kutumia vyema dhima ya kuwepo kwake.

## UCHUMI

### MAANA YA UCHUMI




Zipo tafsri mbali mbali za uchumi ambazo zimetolewa na wanataaluma mbali mbali. Baadhi ya tafsri hizo ni pamoja na;

UCHUMI ni matumizi mazuri ya rasilimali (Kwa lugha ya kiingereza ; Economics is the use of scarce resources).

### MAANA YA MRADI

**Maana ya mradi nini?**
Mradi ni jumla ya shughuli zilizobuniwa kutekelezwa kwa lengo la kutatua tatizo fulani lililojitokeza ndani ya jamii katika kipindi maalum.

Au maana nyingine ya kutafsiri mradi inaweza kuwa;

Mradi unaweza kutafsiriwa kwamba ni shughuli ya uwekezaji, ambapo rasilimali ya fedha imetumika kutengeneza rasilimali mtaji, ambayo itazalisha faida katika kipindi cha muda mrefu.

**Mfano 1:** katika jamii kumeonekana kuwa kuna kukosekana kwa huduma za afya katika eneo fulani na kule ambapo huduma zinapatikana ni mbali, hivyo wana jamii kwa umoja wao wanaibua hilo kama tatizo la msingi kwao na kuona kuwa kuna haja ya kujenga kituo cha afya. Ujenzi wa kituo cha afya ni MRADI ambao unakwenda kutatua tatizo la ukosefu wa huduma za afya.

**Mfano 2:** Katika taasisi kumeonekana kuwa viongozi na wafanya kazi hawana ujuzi wa kutosha kutekeleza majukumu yao, hivyo inaonekana kuwa taasisi iweze kukodi watalaam

washauri waingie mkataba na taasisi kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uongozi ili kuwajengea uwezo viongozi. Kwa mantiki hii, kutoa mafunzo ni MRADI ambao ukawenda kutatua tatizo la ukosefu wa maarifa kwa viongozi.

## MRADI WA KIUCHUMI

Mradi wowote ambao utatumia rasilimali, ni mradi wa kiuchumi. Kama ilivyotafsiriwa hapo juu lengo kuu la mradi ni kutatua tatizo lililopo katika jamii.

## USIMAMIZI WA FEDHA

### MAANA YA USIMAMIZI WA FEDHA

Usimamizi wa fedha ni namna ya kusimamia mapato na matumizi katika biashara ili kutimiza lengo fulani.

Moduli ya stadi za uhasibu na usimamizi wa fedha imefafanua kwa kina zaidi juu ya mada hii.

## MASWALA YA USIMAMIZI WA FEDHA KWA MUJIBU WA KATIBA YA BAKWATA

### UTANGULIZI

Katika katiba ya BARAZA na rasimu za kanuni za jumuiya zake, zipo ibara na vifungu zimeelekeza maswala ya fedha.

### IBARAZA KUTOKA KATIBA YA BARAZA

Zifuataza ni Ibara na vifungu ambavyo vimo katika katiba ya Baraza vinafafanua maswala ya fedha;

**Ibara ya 104:** Baraza Kuu la Waisilam wa Tanzania (BAKWATA) linapata fedha zake za kuendesha shughuli zake mbali mbali kutokana na ;-

1. Michango ya hiari ya Waisilam Wenyewe
2. Miradi mbali mbali ya Baraza Kuu la Waisilam wa Tanzania(BAKWATA) kuanzia ngazi ya Msikiti hadi Taifa.
3. Mifuko maalumu kwa uendelezaji wa shughuli maalumu.
4. Misaada ya fedha taslim kutoka kwa wakarimu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.
5. Mikopo kutoka Mabenki na Taasisi nyingine za fedha ndani na nje ya nchi.

**Ibara ya 105:** Fedha za Baraza Kuu la Waisilam wa Tanzania (BAKWATA) zinazopatikana kutokana na Miradi na Shughuli zake nyingine halali, zitawekwa Benki na zitatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kwa mujibu wa kanuni za fedha zilizowekwa na Baraza kuu la Waisilam wa Tanzania (BAKWATA)

**Ibara ya 106:** Kila mradi wa Baraza kuanzia ngazi ya Msikiti hadi Taifa na utawasilishwa sehemu ya mapato ya mradi huo Bakwata Taifa kulingana na asilimi ya zitakazoanishwa na Halmashauri kuu ya Taifa.

**Ibara ya 107:** Kwa ajili ya kusimamia na kutoa huduma za kawaida za kila siku kwa misikiti na waumini wote wa kiisilam nchini, Misikiti yote Tanzania itawajibika kuchangia kiasi cha shilingi elfu kumi (tsh.10,000), kwa kila mwezi kwa msikiti wa daraja **(C ),** Shilingi elfu ishirini(tsh.20,000) kwa mwezi kwa msikiti wa daraja **(B)** na shilingi elfu thelathini (tsh.30,000) kwa mwezi kwa msikiti wa Daraja **(A).** Michango hiyo italipwa moja kwa moja kupitia benki katika akaunti itakayoelekezwa na Halmashauri Kuu, kisha mlipaji atawasilisha itakavyoelekezwa na Mhasibu wa Wilaya.
**Tanbihi 1:** *Msikiti DARAJA C ni Msikiti unaosaliwa na waumini kati ya 1-50, DARAJA B ni kati ya 51-99 na DARAJA A ni kuanzia 100 na zaidi.*
**Tanbihi 2:** *Gawio kutoka kila Wilaya litawekwa katika akaunti ya MKOA. Mkoa utakuwa na wajibu kutumia fedha hizo kufanya miradi mbali mbali.*
**Ibara ya 108:** Katika kutafuta fedha za kuendesha shughuli zake, Baraza Kuu la Waisilam Tanzania halitatumia njia yoyote ile isiyokuwa ya halali.
**Ibaraza ya 109:** Mwaka wa fedha wa Baraza Kuu la Waisilam wa Tanzania utaanza tarehe 1 mwezi wa Kwanza , na kumalizika tarehe 31 Mwezi wa kumi na mbili '**MILLAADIYAH'**

## MASWALA YA FEDHA KATIKA NGAZI ZA KIUTAWALA ZA BARAZA

Maswala ya kifedha yametajwa katika ibara mbali mbali za ngazi mbali mbali za kiutwala wa BARAZA kanuni hizi zitaongoza maswala haya muhimu na nyeti kwa uhai wa BARAZA. Ngazi ya msikiti, Kata, Wilaya na Mkoa kama zinavyoonyeshwa hapo chini;

- ❖ **NGAZI YA MSIKITI**
- **Ibara ya 15 (Kifungu cha 5 & 7)**

**Kifungu cha 5:**

Kubuni, Kuendesha, Kusaidia Miradi ya Uchumi ya Msikiti, Kukusanya swadaka, zaka na misaada mbalimbali kutoka kwa waumini na wahisani na kuzitia katika vitabu vya kumbukumbu za hesabu.

**Kifungu cha 7:**

Kukadiria na kusimamia Mapato ya Msikiti

- **Ibara ya 20 (kifungu cha 7 )**

**Kifungu 7**:

Kupokea na kuzingatia Taarifa za Mapato na Matumizi ya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania (BAKWATA) katika eneo la Msikiti.

- ❖ **NGAZI YA KATA**
- **Ibara ya 24 (kifungu cha 4 na 6)**

**Kifungu cha 4:**

Kubuni, kuendesha, Kusaidia Miradi ya Uchumi ya Kata, kukusanya swadaka, zaka na misaada mbalimbali kutoka kw waumini na wahisani na kuzitia katika vitabu vya kumbukumbu za hesabu.

**Kifungu cha 6:**

Kukadiria na kusimamia Mapato na Matumizi ya Kata.

- **Ibara ya 30 (kifungu cha 8)**

**Kifungu cha 8**

Kupokea na kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania (BAKWATA) katika Kata mwaka hadi mwaka.

❖ **NGAZI YA WILAYA**

- **Ibara ya 35 (kifungu cha 4 na 5)**

**Kifungu cha 4:**
Kubuni, kuanzisha,kuendesha, Kusaidia Miradi ya Uchumi ya Wilaya, kukusanya swadaka, zaka na misaada mbalimbali kutoka kw waumini na wahisani na kuzitia katika vitabu vya kumbukumbu za hesabu.

**Kifungu cha 5:**
Kukadiria na kusimamia Mapato na Matumizi ya Baraza Kuu la Waisilamu wa Tanzania(BAKWATA) katika Wilaya.

- **Ibara ya 42 (kifungu cha 7)**

**Kifungu cha 7**
Mkutano mkuu wa Wilaya utapokea na kuidhinisha makisio ya Mapato na Matumizi ya Baraza kuu katika Wilaya mwaka hadi mwaka.

❖ **NGAZI YA MKOA**

- **Ibara ya 46 (kifungu cha 6)**

**Kifungu cha 6:**
Kukadiria na kusimamia Mapato na matumizi ya Mkoa

- **Ibara ya 52 (kifungu cha 8)**

**Kifungu cha 8:**
Mkutano Mkuu wa Mkoa utapokea na kuidhinisha makisio ya mapato na matumizi ya mkoa mwaka hadi mwaka.

## MAMBO YANAYOHUSU UHASIBU

### MWAKA WA FEDHA WA BARAZA

Mwaka wa fedha wa BARAZA kama inavyonukuliwa katika katiba ya BARAZA ibara ya 109, utakuwa unaanzia tarehe 1 mwezi wa Kwanza(Januari) , na kumalizika tarehe 31 Mwezi wa kumi na mbili (Disemba) **'MILLAADIYAH'**

### MISINGI YA UHASIBU

Hesabu za BARAZA zitaandikwa kuonesha mapato na matumizi ya fedha na rasilimali zote.
Mali za kudumu zitaorodheshawa kwenye daftari maalumu na mwisho wa mwaka itaandaliwa orodha ya mali zote za kudumu. Uandaaji wa taarifa za fedha za BARAZA utatenganisha hesabu zinazohusu matumizi ya kawaida na matumizi ya mifuko ya maendeleo itakayokuwa imeanzishwa.

Jina lako..................................................

Namba ya usajili........................................

**MAELEKEZO;**

1. **Unatakiwa kujibu maswala YOYOTE 10**
2. **Kila swali lina alama 10 (10%) na hivyo jumla ya alama ni 100 (100%).**
3. **Mtihani huu ni upimaji wa wazi (OPEN BOOK PAPER) hivyo unatakiwa kujibu maswali kwa kutumia upeo wa kujieleza zaidi ili kupima ufahamu wa moduli na siyo kunakili msitari kwa msitari kutoka katika moduli**

MASWALI

1. Wewe ni Kiongozi wa BAKWATA , je unatakiwa ufanye nini ili aweze kuwa kiongozi bora wa BAKWATA halisi ya kumpeleka peponi na siyo BAKWATA ya kujiundia MOTO?
2. (a) Ni yepi madhumuni ya kuwa na katiba ya BAKWATA
   (b) chagua madhumuni matatu ya katiba ya BAKWATA na ufafanue namna yanavyotekezwa katika eneo lako la uongozi.
3. Kwa kutumia mifano yako, orodhesha changamoto tatu zinazokwaza kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika eneo lako unaloongoza na pia weka mapendekezo ya kutatua changamoto hizo.
4. Neno MIPANGO limetajwa mara 13 katika katika katiba ya BAKWATA. Taja nafasi ya cheo chako ndani ya BAKWATA na fafanua ibara ambayo inataja mipango ya cheo chako kwa kufanya ufafanuzi mfupi manvyotekeleza mipango.
5. Baada ya kufahamu hadhi ya BAKWATA kama katiba ilivyoandikwa, taja mambo ambayo unayaona katika uongozi wako yana mapungufu na njia aza kuyaweka sawa.
6. Eleza kwa ufupi utakavyoweza kusaidiana na viongozi wenzako katika utekeleza mipango ya BAKWATA baada ya kusoma moduli hii
7. (a) Waqfu nini?
   (b)Orodhesha chamoto za waqfu nyingi kutotimizwa malengo ya matumizi yake
8. Orodhesha madhara ya kukosekana kwa nidhamu ndani ya BAKWATA
9. Usimamizi wa fedha ni swala la kikatiba katika BAKWATA. Orodhesha ibara za katiba unazotumia katika ngazi yako ya kuongozi kulinda fedha za BAKWATA na fafanua mfumo mzima wa fedha mnavyoutekeleza na wenzako.
10. Kutokana na kauli mbiu ya jitambue, badilika, acha mazoea, je wewe kama kiongozi, fafanua mambo yafutayo;

a) Je, kwa kiasi gani umejitambua?
b) Je, ni tabia zipi unadhani unahitajika kubadilika?
c) Je, ni mambo gani umekuwa ukiyafanya kwa mazoea pasina ujuzi?
d) Andika kwa ufupi sana juu ya kauli mbiu hii inavyokusaidia kuwa kiongozi bora.